# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR



**MHE. HEMED SULEIMAN ABDULLA**
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**



**MHE. DKT. KHALID SALUM MOHAMED**
**WAZIRI WA NCHI AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI**



**ND. THABIT IDAROUS FAINA**
**KATIBU MKUU AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**Dira:**

*“Kuwa na Serikali yenye kutoa huduma bora kwa jamii na yenye uhimili mzuri wa uchumi, umoja na maendeleo endelevu”.*

***Dhamira***

*“Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika sekta zote za SMZ na masuala ya Muungano kwa kufuata misingi ya Katiba na Sheria pamoja na kufuata misingi ya haki za binaadamu na ushirikishwaji”.*

**YALIYOMO**

YALIYOMO........................................................................................ i

UTANGULIZI...................................................................................... 1

PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA
MAKAMU WA PILI WA RAIS ................................................................ 27

PROGRAMU KUU - ((PCO102): URATIBU WA SHUGHULI
ZA SERIKALI...................................................................................... 28

PROGRAMU KUU - (PCO103): UENDESHAJI NA URATIBU WA
AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS .............................................. 39

PROGRAMU KUU - (CO201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA
BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI NA PROGRAMU
KUU – PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA
WA BARAZA LA WAWAKILISHI ......................................................... 45

TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR (C03)...................................... 46

PROGRAMU KUU - (PCO301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA
UCHAGUZI ........................................................................................ 46

PROGRAMU KUU - (CO302): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA
ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI
YA ZANZIBAR.................................................................................... 47

UTEKELEZAJI KIFEDHA.................................................................... 48

MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022................................................. 49

PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA
MAKAMU WA PILI WA RAIS ................................................................ 49

PROGRAMU KUU - (C0102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI ........ 50
PROGRAMU KUU - (CO103): UENDESHAJI NA URATIBU WA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS ........ 57
PROGRAMU KUU - (CO201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI na PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI ........ 61
PROGRAMU KUU - (CO301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI ........ 63
PROGRAMU KUU - (CO301): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA NA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR........ 63
UKUSANYAJI MAPATO........ 64
HITIMISHO ........ 65
VIAMBATANISHO........ 68

**HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na hatimae likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi ili liidhinishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa na kwa unyenyekevu mkubwa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutujaalia afya njema na uhai na kwa uwezo wake anaendelea kutuwezesha kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Aidha, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani na utulivu na kutujaalia mashirikiano na upendo miongoni mwetu.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na wananchi wote wa Tanzania kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17/3/2021 na kuzikwa tarehe 26/3/2021 huko Chato Mkoani Geita. Aidha, natoa pole kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk Hussein Ali Mwinyi na wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla kwa kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad aliyefariki tarehe 17/2/2021 na kuzikwa tarehe 18/2/2021 huko Mtambwe Pemba. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu wapendwa wetu hawa mahala pema peponi….Amin.

4. **Mheshimiwa Spika,** mauti ni haki na ni safari ya kila mmoja wetu, bila shaka wao wametangulia na sisi tupo nyuma yao. Hatutowasahau daima kwa mema waliyoitendea nchi yetu pamoja na uongozi wao uliotukuka uliokuwa na azma ya kulipeleka Taifa hili kwenye mafanikio makubwa. Sisi tuliobakia tutayaendeleza kwa dhati yale yote waliyodhamiria kuyafanya na kusimamia katika nchi yetu. Baada ya kusema hayo Mheshimiwa Spika kwa ridhaa yako sasa ***nawaomba tusimame kwa dakika moja kwa ajili ya kuwakumbuka na kuwaombea viongozi wetu hawa.***

5. **Mheshimiwa Spika,** baada ya salamu hizo za pole, sasa napenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais. Tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awazidishie nguvu, hekma, busara na uimara wa kuiongoza nchi yetu ili kufikia katika uchumi wa juu.

6. **Mheshimiwa Spika,** pia, nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa namna anavyoendelea kuiongoza nchi yetu kuelekea katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu, afya, hekima na busara katika uongozi wake na kuweza kuifikia azma aliyo nayo ya kuipa maendeleo makubwa nchi yetu. Aidha, kwa namna ya kipekee nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Viongozi wetu Wakuu wa Zanzibar wa Awamu ya Saba Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa namna walivyoiongoza nchi yetu na kuweza kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa mafanikio makubwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape afya njema na mapumziko mazuri pamoja na familia zao.

7. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, shukurani za pekee zije kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa namna unavyoliongoza Baraza hili la Wawakilishi na kwa wasaidizi wako pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa namna walivyoanza vyema katika kuwatumikia wananchi katika kazi yao hii. Bila shaka tutaendeleza wajibu wetu huu ili tuweze kuleta maendeleo katika majimbo yetu na Zanzibar kwa ujumla.

8. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa ridhaa yako sasa naomba nieleze kwa muhtasari hali ya masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Bila shaka masuala hayo yataelezwa kwa undani zaidi na Waheshimiwa Mawaziri wakati watakapowasilisha hotuba zao za bajeti.

## Hali ya Uchumi wa Zanzibar

### *Hali ya Ukuaji wa Uchumi*

9. **Mheshimiwa Spika,** kama tunavyoelewa tangu mwanzoni mwa mwaka 2020, dunia imekuwa katika mtihani mkubwa wa kuwepo kwa janga la maradhi ya mripuko ya Covid – 19. Kutokana na juhudi mbalimbali zilizochukuliwa kukabiliana na janga hilo, shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii duniani zimezorota ikiwemo uwekezaji na uzalishaji, kufungwa kwa mipaka na kusababisha kuporomoka kwa soko la utalii, kuongezeka matumizi ya Serikali katika miradi ya afya kuliko miradi mingine ya maendeleo, kupoteza wananchi wengi kwa vifo pamoja na kusimama kwa miradi mingi ya maendeleo.

10. **Mheshimiwa Spika,** wakati uchumi wa dunia ukiporomoka kufikia wastani wa asilimia 3.3 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2019 na uchumi wa nchi za Afrika ukiporomoka kufikia wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2020 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2019. Uchumi wa Zanzibar umekua katika kipindi cha mwaka 2020 na ikiwa ni miongoni mwa nchi 11 katika bara la Afrika zilionesha ukuaji wa uchumi ingawa kwa kasi ndogo katika kipindi cha mwaka 2020.

11. **Mheshimiwa Spika,** Uchumi wa Zanzibar umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2019. Kasi hii ya ukuaji katika kipindi hiki pamoja na mambo mengine imetokana na kuongezeka kwa ukuaji wa sekta ndogo ya kilimo kufikia wastani wa asilimia 1.5 na ongezeko la samaki waliovuliwa ambao wamefikia tani 38,107.0 mwaka 2020 kutoka jumla ya tani 36,728.0 mwaka 2019. Vile vile, kumekuwa na ongezeko la ajira serikalini kufikia jumla ya ajira 41,892 kutoka ajira 38,795 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 7.9. Aidha, shughuli za ujenzi zimeongezeka kwa kufikia asilimia 6.5 mwaka 2020 kutoka asilimia 3.1 mwaka 2019 ikichangiwa zaidi na kuendelea kwa ujenzi wa miradi ya maendeleo ikiwemo barabara, viwanja vya ndege, vituo vya afya na miradi mengine ya utoaji huduma.

12. **Mheshimiwa Spika,** sababu nyengine ni kuimarika kwa utoaji huduma kutoka Serikalini kufikia wastani wa asilimia 13.2 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 11.5 mwaka 2019, kuongezeka kwa huduma ya elimu kufikia wastani wa asilimia 9.7 kutoka wastani wa asilimia 7.5 mwaka 2019 pamoja na kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la karafuu katika kipindi cha mwaka 2020 kufikia jumla ya tani 3,506.8 kutoka tani 1,744.9 mwaka 2019.

13. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio yote hayo yanatokana na kuendelea kuwepo kwa hali ya amani na utulivu nchini jambo ambalo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi.

***Pato la Taifa na Pato la Mwananchi***

14. **Mheshimiwa Spika,** Pato halisi la Taifa limeendelea kuwa zuri ambapo kwa mwaka 2020 lilifikia thamani ya **Shilingi 3,116** bilioni ikilinganishwa na thamani ya **Shilingi 3,078** bilioni mwaka 2019. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za soko limefikia thamani ya Shilingi **4,209** bilioni mwaka 2020 kutoka thamani ya **Shilingi 4,136** bilioni mwaka 2019. Hali iliyosababisha Pato la Mwananchi kufikia **Shilingi 2,526,000** sawa na Dola za Kimarekani 1,099 kutoka **Shilingi 2,551,000** sawa na Dola 1,115. Kipato hiki kimeifanya Zanzibar iendelee kubaki katika nchi za

uchumi wa kiwango cha chini cha kati. Kupungua kwa Pato la mwanchi mmoja mmoja kumetokana na kukua kwa kasi ndogo ya uchumi na kuongezeka kwa idadi ya watu.

*Mfumko wa Bei*

15. **Mheshimiwa Spika,** kasi ya mfumko wa bei za bidhaa na huduma nchini imeongezeka hadi kufikia wastani wa **asilimia 3.4** mwaka 2020 ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 2.7** mwaka 2019. Kupanda huko kumesababishwa na kupanda kwa bei za bidhaa zote za chakula. Bidhaa za chakula zilitoka wastani wa **asilimia 2.8** mwaka 2019 hadi kufikia wastani wa **asilimia ¬5.8** mwaka ¬2019. Aidha, bidhaa zisizo za chakula zimeshuka kutoka wastani wa **asilimia 2.6** mwaka ¬2019 na kufikia wastani wa **asilimia ¬ 1.7** mwaka ¬2020.

*Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2021*

16. **Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2021 unategemea kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

17. **Mheshimiwa Spika,** Pato la Taifa lilitarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa baina ya asilimia 4 – 6 kwa mwaka 2020 kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwemo kuanza miradi mikubwa ya kipaumbele na maendeleo, kuwa na sera nzuri na jumuishi za uwekezaji pamoja na kuweka mifumo imara ya ukusanyaji kodi. Hata hivyo, kutokana na kuendelea kuwepo kwa janga la ugonjwa wa COVID 2019 duniani, ¬uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2021 unatarajiwa kukua kwa kasi ya chini ya asilimia 5.2. Hii ni kutokana na hali ya uchumi duniani iliyosababishwa na athari za Ugonjwa wa COVID 19 ambao umeathiri sekta za uchumi ikiwemo utalii, biashara na uwekezaji.

**Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali**

**18. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuchukuwa hatua madhubuti za kuhakikisha mapato ya Serikali yanaongezeka ili kuweza kugharamia matumizi mbalimbali ya Serikali ikiwemo huduma za kijamii. Mbali na kuongeza vyanzo vipya vya kukusanya mapato, Serikali imeongeza usimamizi na ufuatiliaji katika maeneo yetu ya ukusanyaji mapato sambamba na kudhibiti uvujaji wa mapato hayo katika maeneo yote. Jithihada hizo na hatua zilizochukuliwa tayari zimeonesha mafanikio ambapo takwimu zinaonesha kuwa kumekuwa na muendelezo wa ongezeko la Mapato ya Serikali katika kipindi cha miezi sita iliyopita ambapo katika kipindi cha Januari - Machi 2021 zimekusanywa **Shilingi Bilioni 236.2** kutoka **Shilingi Bilioni 206.7** za Oktoba - Disemba 2020 na **Shilingi Bilioni 153.9** za kipindi cha Julai - Septemba 2020.

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa upekee naomba kuchukuwa nafasi kulipongeza Shirika la Bandari Zanzibar kwa hatua kubwa waliofikia katika kukusanya Mapato kwa kipindi hiki kifupi ambapo kumekuwa na muendelezo wa ongezeko la makusanyo katika Shirika hilo. Takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha Julai - Septemba 2020 Shirika lilikusanya **Shilingi Bilioni 7.9** na kuongeza hadi **Shilingi Bilioni 8.5** katika kipindi cha Oktoba - Disemba, 2020. Ongezeko jengine lilishuhudiwa katika kipindi cha Januari - Machi, 2021 la Shilingi Bilioni 9.4. Bila shaka ongezeko hili la mapato linaenda sambamba na faida inayopatikana ambayo inachangia katika mfuko mkuu wa Serikali. Katika vipindi hivyo Shirika limepata faida ya **Shilingi Bilioni 2.8**, **Shilingi Bilioni 4.3** na **Shilingi Bilioni 5.5** kwa kila kipindi.

**20. Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukuwa nafasi hii kuzisisitiza Idara, Taasisi na Mawizara yetu yanayokusanya mapato kuzidisha kasi ya ukusanyaji na kuondokana kabisa kuvujisha mapato hayo. Bado huduma za Serikali kwa Wananchi wake zinategemea sana mapato yetu ya ndani, hivyo kila mmoja wetu anawajibu wa kuhakikisha mapato yetu yanaongezeka kila mwaka ili tuzidi kupunguza utegemezi wa fedha kutoka nje.

**Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2021/2022**

21. **Mheshimiwa Spika,** ili kuwa na dira ya kufikia katika maendeleo tunayoyahitaji, Serikali imeweka Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo ambao utazingatia malengo na mikakati inayotokana na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 ambayo inalenga, kuifikisha Zanzibar katika Kiwango cha Juu cha Uchumi wa Kati kupitia mihimili mikuu minne ambayo ni Mageuzi ya kiuchumi; Maendeleo ya rasilimali watu na huduma za kijamii; Kuimarisha miundombinu; na Utawala bora na uhimili. Aidha, Mwelekeo huu umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025, Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi, ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa wananchi wakati wa Kampeni za Uchaguzi, Maelekezo ya Serikali kiujumla pamoja na miongozo iliyotolewa na viongozi wakuu kupitia sekta tofauti. Ili kufikia azma hiyo, Serikali imefanya uchambuzi wa programu na miradi mbalimbali na kuelekeza kuanza kwa taratibu za kuiendeleza miradi hiyo kwa njia tofauti na kuiweka katika maeneo manne kama ifuatavyo:-

(i) Miradi ya kipaumbele itakayotekelezwa na Serikali na Washirika wa Maendeleo kwa mwaka 2021/2022 ambayo ni ile inayoendana na dhana ya uchumi wa buluu, kuimarisha mapato na maendeleo ya uchumi na huduma za kijamii kwa ujumla. Programu na miradi katika eneo hili ni pamoja na Kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa Bandari ya Mangapwani na Mpigaduri; Ununuzi wa meli 4 za uvuvi; Kuendelea na uwekaji wa miundombinu ya maji katika visima vya Ras el Khaimah; Kuendelea na ujenzi wa Hospitali Mpya ya rufaa na kufundishia Binguni; Kuendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana; na Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kidijitali ya utendaji kazi kwa ujumla, ukusanyaji mapato, usimamizi wa matumizi, manunuzi na utunzaji wa kumbukumbu za usajili wa mali za umma.

(ii) Miradi itakayotekelezwa kwa ubia katika kuimarisha dhana ya mashirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi. Maeneo yalikusudiwa kuwemo katika kundi hili ni pmoja na Kuendeleza Uwanja wa Biashara na Maonyesho ya Kimataifa Zanzibar (Nyamanzi); Ujenzi wa masoko na stendi maeneo ya Chuini (Kwanyanya), Jumbi, Mkokotoni, Machomane na Ng'ombeni; Kuendeleza sekta ya maziwa; Uvunaji wa maji ya mvua kupitia ujenzi wa makinga maji; na Ujenzi wa kituo cha usarifu na uhifadhi wa bidhaa za samaki.

(iii) Miradi inayopendekezwa kutekelezwa na sekta binafsi ni miradi katika maeneo ya Ujenzi wa nyumba za makaazi; Ujenzi wa viwanda vya mwani; Kuongeza thamani ya zao la dagaa; Kuanzisha mashamba ya kufugia samaki na Kuanzisha mashamba ya kibiashara ya kufugia majongoo bahari.

(iv) Miradi ya kipaumbele inayopendekezwa kufanyiwa Upembuzi Yakinifu (Feasibility Study) ambayo sekta husika zinapaswa kuanza kutayarisha maandiko ya miradi hiyo ambayo inajumuisha Kuanzisha vituo vya kulelea na kukuza wajasiriamali katika kila mkoa, Unguja na Pemba; Kuanzisha na kuendeleza maeneo ya Viwanda (Industrial Parks); Uanzishwaji wa viwanda bunifu vya kuchakata mazao na matunda na mboga mboga (Agro processing innovation hub); Uimarishaji wa kituo cha kisasa cha taarifa (Data centre) kwa kuondoa vifaa chakavu na kuweka mifumo mipya; Ujenzi wa kiwanda cha dawa na Ujenzi wa kituo cha uchunguzi wa maradhi yatokanayo na kazi.

**22. Mheshimiwa Spika,** Miradi ilio katika kundi la kwanza itatekelezwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2021/2022 na ya makundi mengine itatekelezwa kuanzia mwaka 2021/2022 au miaka ya mbele.

**Sekta ya Uchumi wa Buluu**

23. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya Awamu ya Nane imedhamiria kuijenga Zanzibar mpya yenye uchumi wa kisasa kwa kuzingatia matumizi na usimamizi endelevu wa bahari na rasilimali zake pamoja na ukanda wa pwani kwa jumla. Itakumbukwa vyema wakati wa uzinduzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi katika hotuba yake Mheshimiwa Dk Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, moja ya ahadi yake kubwa aliyoitoa kwa wananchi na ambayo pia imeelezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni kujenga uchumi wa kisasa kwa maana ya Uchumi wa Buluu (Blue Economy). Alisema kuwa Uchumi wa Buluu ama uchumi wa bahari unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, matumizi bora ya rasilimali mbalimbali za bahari pamoja na shughuli za utalii wa fukwe na michezo ya baharini. Hivyo, Serikali itaendelea kusimamia, kuratibu na kuimarisha maendeleo ya Uchumi wa Buluu Zanzibar ikiwemo uvuvi na utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

24. **Mheshimiwa Spika,** tayari Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeongeza nguvu kwenye uwekezaji, ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya uchumi wa buluu ikiwemo utafutaji wa mafuta na gesi asilia; ujenzi wa bandari mpya za uvuvi; uimarishaji wa uvuvi wa bahari kuu, ujenzi wa mitambo na viwanda vya kuhifadhi, kusarifu na kuchakata dagaa na samaki pamoja na ujenzi wa miundombinu ya uvuvi wa matenga (Fish Cage Farming).

25. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) inaendelea na Mradi wa Ujenzi wa Diko na Soko la Samaki, Malindi ulioanza mwaka 2019. Mradi huu unaotarajiwa kugharimu jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 14.7 hivi sasa umefikia asilimia 55 ya ujenzi wake ambao takriban mwaka mmoja ulisimama kutokana na kuibuka kwa maradhi ya Covid 19 duniani kote. Mradi unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa kwa Serikali mwishoni mwa mwaka wa fedha wa 2021/2022.

26. **Mheshimiwa Spika,** kumalizika kwa mradi kutasaidia wananchi kuuza na kununua samaki katika mazingira yanayozingatia usafi na usalama. Aidha, mradi huu unatarajia kuzalisha ajira zaidi ya 6,500 kwa wananchi wetu watakaotoa huduma mbalimbali katika diko na soko hilo.

27. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Shirika la Kimataifa la Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) itatekeleza lengo la ununuzi wa meli mpya nne za kisasa za uvuvi. Meli hizo pia zitashirikisha wataalamu kutoka nje kwa lengo la kujenga uwezo wa wavuvi wetu wa Zanzibar. Aidha, mkazo mkubwa pia umewekwa katika kuendeleza ufugaji wa mazao ya baharini kama vile samaki, kaa, pweza, majongoo bahari na ukulima wa mwani.

28. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imejipanga kuisimamia vyema sekta hii na wananchi wapo tayari kutekeleza na kunufaika na matokeo chanya yanayotokana na uchumi wa buluu. Ni matumaini yetu kuwa wakati tunaendelea na shughuli hizo, uchumi wetu utakua kwa kasi na maendeleo katika sekta mbalimbali yatapatikana ikiwemo kuimarika zaidi huduma za kijamii.

29. **Mheshimiwa Spika,** nitoe wito kwa wananchi wenzangu kwa vile nchi yetu imezungukwa na bahari na rasilimali zake ni vizuri kuiona dhana ya uchumi wa buluu kama fursa kwa mabadiliko ya kiuchumi. Ni vyema tukaiunga mkono Serikali yetu katika utumiaji mzuri wa rasilimali hiyo. Katika ulimwengu wa sasa uchumi wa buluu ni kati ya maeneo yanayoangaliwa kwa jicho la kipekee nasi tuendelee kuitumia dhana ya uchumi wa buluu kama mkakati wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu si kwa mtu mmoja mmoja tu bali kwa Taifa kwa ujumla.

**Uimarishaji Uchumi na Maendeleo ya Uwekezaji**

30. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kusimamia masuala ya uwezeshaji na uwekezaji nchini, Serikali itaendelea kutekeleza sheria na miongozo ya kazi; upatikanaji wa ajira za staha hasa kwa vijana na kuimarisha programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua ya kuimarisha huduma za uwekezaji nchini, Serikali imeimarisha utoaji wa huduma kwa kuweka Kituo cha Huduma Jumuishi (One Stop Center) ambapo taasisi zinatoa huduma kwa mashirikiano katika kituo kimoja. Taasisi hizo ni ZIPA, Uhamiaji, Kamisheni ya Ardhi, Kamisheni ya Kazi, Bodi ya Mapato, Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na Kamati ya Udhibiti na Usimamizi wa Ujenzi (DCU). Kituo hiki kinatoa huduma za vibali vya kazi na ukaazi, vibali vya ujenzi, usajili wa makampuni na huduma za kodi na mazingira kwa wawekezaji. Kituo hiki kimefanikiwa kupunguza urasimu na muda wa upatikanaji wa vibali vya kazi na ukaazi kutoka wiki tatu hadi wiki moja kwa wawekezaji. Tunaamini kuwepo na kufanyakazi kwa kituo hiki pamoja na mfumo wa kielektroniki wa kusajili wawekezaji unaoandaliwa na ZIPA kutasaidia zaidi kuondoa urasimu na usumbufu kwa wawekezaji wetu.

32. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeazimia kukifanya Kisiwa cha Pemba kuwa ni Kisiwa cha Uwekezaji Maalum. Tayari Serikali ipo katika hatua ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar namba 14 ya mwaka 2018 ili kuenda sambamba na azma hiyo. Jadweli nambari tatu na nambari sita za Sheria hiyo yamefanyiwa marekebisho ili kuweka vivutio maalum kwa uwekezaji Pemba. Serikali inaendelea kuweka mifumo na taratibu mbalimbali itakayowavutia wafanyabiashara wakubwa wa nje na ndani ya nchi kuwekeza kisiwani Pemba. Tunaamini uwekezaji huo utakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya wananchi wa kisiwa cha Pemba na Zanzibar kwa jumla.

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa suala la ajira kwa vijana bado limekuwa ni miongoni mwa vipaumbele vyetu. Katika kufikia azma yetu ya ajira 300,000 kwa kipindi cha miaka mitano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imeanza kuchukua hatua kwa kuratibu upatikanaji wa ajira katika maeneo mbalimbali. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi wa Machi 2021, Serikali imeratibu upatikanaji wa ajira 1,272 (Wanaume 603 na Wanawake 669) ndani ya nchi katika sekta binafsi za

hoteli, viwanda, skuli binafsi na ulinzi. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Wakala Binafsi wa Ajira imeweza kuratibu upatikanaji wa ajira 842 kwa vijana wetu (Wanaume 59 na Wanawake 783) katika nchi mbalimbali ikiwemo Oman, Qatar na Dubai kwa kazi za ulezi wa watoto, udereva, ulinzi, upishi na kazi za nyumbani.

34. **Mheshimiwa Spika,** Serikali vilevile kupitia Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeendelea kutoa mikopo kwa makundi mbalimbali ya wananchi ili kuweza kuanzisha na kuimarisha shughuli za kiuchumi. Hadi sasa jumla ya mikopo 617 yenye thamani ya Shilingi 637,425,000 (Pemba 221,900,000 na Unguja 405,525,000) imetolewa. Mikopo hiyo hutolewa ama kwa vikundi au mtu mmoja mmoja. Pia, kupitia Idara ya Vyama vya Ushirika vimesajiliwa Vyama vya Ushirika 318 (Unguja: 155; Pemba: 163) ikiwemo SACCOS moja. Tunaamini vikundi hivi vyote vinatoa mchango mkubwa katika kuongeza ajira kwa wananchi wetu na kuwaongezea kipato cha kukidhi mahitaji yao hasa yale ya muhimu.

35. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Serikali kupitia Kamisheni ya Kazi imewapatia vibali vya kazi jumla ya wageni 1,129 kutoka mataifa mbali mbali yakiwemo Italia, India, China, Uingereza na Nchi za Afrika ya Mashariki ili kuweza kufanya kazi hapa nchini.

**Uanzishaji wa Maeneo ya Viwanda**

36. **Mheshimiwa Spika,** katika azma yake ya kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi wake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepanga kuanzisha Maeneo ya Viwanda (Industrial Parks) katika kila Wilaya za Zanzibar nje ya utaratibu wa ZIPA. Kupitia mradi huu unaosimamiwa na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, maeneo hayo yatawekewa miundombinu yote wezeshi kwa ajili ya viwanda vinavyotarajiwa kujengwa na kufanyakazi. Mpaka sasa maeneo matatu (3) ya viwanda tayari yameshatengwa ambayo ni Eneo la Viwanda la Chamanangwe, Eneo la Viwanda la Nungwi na Eneo la Viwanda la Dunga. Serikali tayari imeanza kuliwekea miundombinu muhimu eneo la Chamanangwe lililoko Wilaya ya Wete, Pemba ikiwemo huduma ya umeme, maji na barabara.

37. **Mheshimiwa Spika,** maeneo yote matatu (3) yatakuwa yakiendelezwa hatua kwa hatua kadri ya fedha zitakapopatikana na Serikali inaendelea kufanya mazungumzo na washirika wa maendeleo ili kwa pamoja tuweze kuweka miundombinu yote muhimu katika maeneo haya na mengine yatakayowekwa katika kila Wilaya.

**Zao la Karafuu**

38. **Mheshimiwa Spika,** zao la karafuu bado linaendelea kuwa moja ya vielelezo vya utambulisho wa Zanzibar na ni moja kati ya vyanzo vyetu vikuu vya fedha za kigeni. Aidha, zao hili limekuwa tegemeo kubwa kwa wakulima kupata fedha na kuendeleza shughuli na mahitaji yao ya kiuchumi na kijamii.

39. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali ya uchumi duniani kuendelea kushuka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kusambaa kwa maradhi ya Covid – 19 na kuongezeka kwa nchi zinazozalisha zao hilo duniani, soko la karafuu nalo limekuwa likitikisika kwa kupanda na kushuka. Licha ya hali hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kuwa mnunuzi pekee wa zao hilo hapa nchini kutoka kwa wakulima ili kuweza kulidhibiti na kulisimamia ipasavyo kiuzalishaji na kiubora.

40. **Mheshimiwa Spika,** katika usimamizi huo, Serikali imeamua kutumia utaratibu wa mkulima kulipwa asilimia 80 ya bei ya soko la dunia. Kupitia utaratibu huu, baada ya Serikali kuuza karafuu hizo, iwapo karafuu imeuzwa kwa bei zaidi ya iliyonunuliwa kutoka kwa mkulima, mkulima huyo atalipwa tofauti ya bei iliyouzwa karafuu yake. Hata hivyo, Wananchi wafahamu zao hili litakwenda kibiashara zaidi kutokana na soko la dunia litakapokuwa. Suala la uwazi wa bei litatolewa taaluma zaidi.

41. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hayo, Serikali itaendelea na jitihada za kutafuta masoko zaidi ya karafuu duniani ili karafuu zote zinazozalishwa ziwe na soko la uhakika na pia kupata bei nzuri. Aidha, Serikali itaendelea kutafuta wawekezaji watakaoweza kuanzisha viwanda vya kusarifu karafuu ili kuiongezea thamani karafuu yetu. Vilevile, tutakiimarisha

Kiwanda chetu cha Makonyo kilichopo Pemba ili kiweze kuzalisha bidhaa nyingi zaidi na zenye ubora wa kimataifa.

42. **Mheshimiwa Spika,** Niwaombe wakulima wetu wa karafuu kuzidisha juhudi za kutunza ubora wa karafuu zao ili ziendelee kuwavuta wanunuzi wetu katika soko la dunia na Serikali kwa upande wake itahakikisha inaweka miundombinu ya zao hilo ikiwemo mikopo kwa wakulima, utoaji wa miche ya mikarafuu bila ya malipo, ujenzi na ukarabati wa vituo vya ununuzi, huduma ya bima kwa wanaopata ajali wakati wa uchumaji karafuu, ujenzi wa barabara maeneo yanayozalisha karafuu kwa wingi na elimu kwa wakulima.

**Maendeleo ya Sekta ya Utalii**

43. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imechukua hatua za kimkakati ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Utalii inaimarika na kuleta tija zaidi katika nchi yetu. Serikali inaendelea kufanya mikutano inayohusu masuala ya utalii kwa njia ya mitandao ***(zoom meeting)*** kutokana na kuendelea kwa janga la maradhi ya Covid - 19 duniani. Mikutano hiyo iliyofanywa ni pamoja na Shirika la Ndege la KLM, Giant Tour Operator ya Marekani, Tanzania Qatar Business Forum na Russia Tanzania Cultural Center pamoja na Afisi zote za Kibalozi za Tanzania zilizoko nchi za nje. Mikutano hii imesaidia katika kuhakikisha kuwa ramani ya Zanzibar kama kituo cha utalii inaendelea kubakia kwenye macho na mawazo ya wasafiri ulimwenguni kote pamoja na kudhibiti masoko yetu ya utalii ya asili na kuibua masoko mapya. Serikali pia imeandaa muongozo wa kuendesha shughuli za utalii nchini kwa kuzingatia uwepo wa maradhi ya Covid – 19 duniani ili kuendelea kuikinga nchi yetu na maambukizi ya Korona lakini pia kuwahakikishia wageni kuwa wanatembelea eneo salama.

44. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, Serikali inaendelea kuvitangaza vivutio vyetu vya utalii vilivyopo Zanzibar ndani na nje ya nchi kwa njia ya picha (vitual) pamoja na kuratibu mafunzo ya kitaalamu ya habari za kitalii kwa waandishi wa habari 18. Waandishi watano (5) wanatoka

Kampuni ya 24 Travel Channel ya Urusi, waandishi wanne (4) kutoka Kampuni ya Russian TV, waandishi sita (6) kutoka Nile TV International ya Misri na waandishi watatu (3) kutoka kampuni ya Botravail ya nchini Ufaransa. Waandishi hao walifanikiwa kutengeneza filamu kutoka kwenye vivutio vya utalii na kuzionesha filamu hizo kwenye televisheni za nchi zao ili kuitangaza zaidi Zanzibar na kuongeza idadi ya wageni wanaokuja nchini kwetu. .

45. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa dhana ya utalii kwa wote, Serikali imewahamasisha Wazanzibari kuwekeza katika sekta ya utalii na tunashukuru dhana hiyo imeitikiwa kwa kiasi kikubwa. Kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, jumla ya miradi 60 ya wazalendo imeanzishwa ikiwemo nyumba za kulaza wageni, kampuni za kuandaa misafara ya watalii, mikahawa na kampuni za michezo ya baharini. Miradi hii vilevile imesaidia katika kutoa ajira za moja kwa moja kwa jamii yetu.

46. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kupanga mikakati mizuri ya ukuzaji utalii wetu kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuendelea kufanya tafiti za utokaji wa wageni pamoja na kufanya ukaguzi wa miradi ya utalii na doria katika maeneo ya utalii, kuendelea kutoa mafunzo kwa watoa huduma za utalii na masheha juu ya sheria na kanuni ili kuboresha huduma wanazozitoa kwa wageni na kutoa mafunzo juu ya njia bora za kufanya utalii kwa manufaa ya nchi yetu. Wito wangu kwa wanaotoa huduma za utalii kuendelea kushirikiana na Serikali kwa namna zote katika kuiendeleza sekta hii muhimu ambayo ina tija kubwa kwa nchi yetu.

47. **Mheshimiwa Spika,** suala la utalii linaendana sana na kuitangaza Zanzibar kihistoria na kitamaduni. Katika kuiunganisha historia ya Zanzibar na utalii, Serikali imefanya utafiti mdogo na kuweza kupata taarifa za historia kwa maeneo ya Chemchem, kwa Mazinge na Shangani yaliyopo Mkokotoni (Unguja) na utafiti juu ya mji wa Mkumbuu kwa Pemba kwa lengo la kutaka kuurudisha katika hali yake ya awali na kuweza kuvutia zaidi. Vilevile tunaenedelea kuyatangaza maeneo yetu ya kihistoria ndani na nje ya nchi kwa kuchapisha vipeperushi pamoja

na kuweka mabango ya maelezo ambayo yatasidia kufahamika kwa historia katika maeneo ya kihistoria kama Bungi, Mvuleni, Mtoni na Maruhubi.

48. **Mheshimiwa Spika,** nitoe wito kwa Wizara inayosimamia Mambo ya Kale kuendelea kutoa ushauri wa kitaalam, kusimamia kwa ukaribu zaidi miradi ya Uhifadhi wa Majengo na maeneo ya wazi kwa mujibu wa Mpango Mkuu wa Uhifadhi (Conservation and Heritage management Plan), kushirikiana na sekta binafsi katika uhifadhi na uendelezaji wa Mji Mkongwe kwa kuufanya Mji huu kuwa kivutio zaidi cha utalii na kuongeza Pato la Taifa pamoja na kuzidi kutoa elimu kwa wananchi na kuwataka kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Sekta ya Utalii ili kufikia azma ya Serikali ya "Utalii kwa Wote"

**Upatikanaji wa Maji Safi na Salama pamoja na Umeme**

49. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora ya maji safi na salama imefanikiwa kurejesha huduma hiyo katika baadhi ya maeneo baada ya kufanya matengenezo katika visima vilivyokuwa na hitilafu Unguja na Pemba. Jumla ya visima 25 vimefanyiwa matengenezo kati ya visima 85 kwa Unguja na Pemba sambamba na kuzifanyia matengenezo pampu na Mota 9. Aidha, jumla ya pampu 8 zimenunuliwa na kufungwa katika Kisima cha Kiembe Samaki kwa Bakathir, Bumbwini Kidanzini, Mfenesini, Bumbwisudi NB5, NB7, NB8, Bumbwini Uwandani na Kiashange JP5 – 2. Pampu hizo hivi sasa zinafanyakazi na kusambaza maji katika maeneo hayo na maeneo mengine.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza juhudi za kutunza na kuhifadhi vianzio vya maji, Serikali imefanikiwa kuyalinda kwa kuyawekea uzio maeneo 86 kati ya 315 kwa Unguja na Pemba. Vilevile Serikali imefanikiwa kutafuta Hatimiliki za maeneo ya visima na vyanzo vya maji ambapo maeneo 67 yamepatiwa hati miliki kati ya maeneo 302 kwa Unguja na Pemba.

51. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora ya maji safi na salama. Hivi sasa inaendelea kutekeleza mradi mkubwa wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Maji Zanzibar (Rehabilitation and Improvement of Water Supply System in Zanzibar – ***"RIWSSZ"***) wenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 92.18. Mradi huu unatarajiwa kuchimba visima 64 vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya lita 792,000 kwa saa na kujenga matangi 14 ( 7 ya ardhini yenye uwezo wa kuhifadhi lita 101 milioni kwa siku na 7 ni matangi ya juu yenye uwezo wa kuhifadhi lita 54.45 milioni kwa siku). Tunaamini baada ya kukamilika kwa mradi huu utakaohusisha maeneo ya Wilaya za Magaribi A, Magharibi B na Kati kutakuwa na upatikanaji endelevu wa maji safi, salama na ya kutosha na kwa gharama nafuu kwa watu na sekta zote katika maeneo husika. Aidha, kupitia mradi huu kutakuwa na utaratibu wa kutumia teknolojia za usimamizi wa rasilimali maji zenye kuzingatia utunzaji wa mazingira, kwa kukuza uchumi, ustawi wa jamii na maendeleo endelevu.

52. **Mheshimiwa Spika,** licha ya jitihada hizo, bado natoa wito kwa Mamlaka ya Maji – ZAWA kujitahidi kutumia vifaa bora katika miundombinu yao ya usambazi maji kwani kumebainika hitilafu nyingi katika miundombinu yao hali inayosababisha kuvuja kwa maji na wakati mwingine wananchi kukosa maji kabisa licha kuwepo kwa miundombinu. Aidha, ni vyema wakawatathmini upya wakandarasi wao kwa miradi mbalimbali juu ya uwezo wao wa kutoa huduma waliokubaliana.

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa huduma za umeme, Serikali kupitia Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) imefanikiwa kupunguza maeneo yanayopata matatizo ya umeme mdogo Unguja na Pemba. Katika kipindi hiki jumla ya maeneo 29 kati ya 64 kwa upande wa Unguja na tisa (9) kati ya 52 kwa upande wa Pemba yameondokana kabisa na tatizo hilo. Aidha, Shirika limefanikiwa kupeleka umeme katika vijiji 29 Unguja na vijiji 20 Pemba. Pamoja na mambo mengine, usambazaji wa umeme katika vijiji vingi kumetokana na punguzo kubwa la ada ya uunganishaji umeme kutoka Shilingi 460,000 hadi Shilingi 200,000.

**54. Mheshimiwa Spika,** tangu kuanzishwa kwa utaratibu huu, hadi mwishoni mwa mwezi wa Machi 2021, jumla ya wananchi 10,410 kutoka maeneo mbalimbali hasa ya vijijini wameungiwa umeme ambapo katika kipindi hicho kwa bei ya awali inakisiwa wanachi 4,850 tu ndiyo wangehudumiwa. Jihada zote hizi zinachukuliwa ili kuweza kuyafikia maeneo yote ya Zanzibar kwa kuyapa huduma bora za umeme.

**Huduma za Afya**

**55. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inaendelea kusimamia sera yake ya kuwa wananchi wanapata huduma za afya bila ya gharama yoyote kama inavyostahiki. Hivyo, jitihada mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ili upatikanaji wa huduma hii uwe endelevu ikiwa ni pamoja na kujenga na kuvifanyia matengenezo vituo vya afya pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wetu wa afya kwa lengo la kuwawezesha kutoa huduma sahihi kwa wagonjwa.

**56. Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanikiwa kutekeleza mikakati mbalimbali ili kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vinanavyotokana na uzazi na vifo vya watoto wachanga. Miongoni mwa juhudi zinazochukuliwa ni kufanya uhakiki wa vifo hivyo ili kubaini sababu zilizopelekea na kuchukua hatua stahiki. Aidha huduma za chanjo kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja zinaendelea kutolewa katika vituo vya afya Unguja na Pemba ili kuwakinga na maradhi mbalimbali hatarishi.

**57. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ugonjwa wa malaria, tunashukuru Mungu unaendelea kudhibitiwa na kubakia chini ya asilimia moja. Hata hivyo, yapo baadhi ya maeneo ambayo hutoa wagonjwa zikiwemo Wilaya za Mjini, Magharibi ‘A’ na Magharibi ‘B’. Katika kipindi hiki cha utekelezaji, jumla ya wagonjwa 440,715 walichunguzwa vimelea vya malaria, kati yao wagonjwa 2,626 sawa na asilimia 0.6 waligunduliwa kuwa na vimelea hivyo na wote walipatiwa matibabu stahiki. Serikali inaenandelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari za kujikinga ikiwemo kutumia vyandarua na kutoa ushirikiano wakati wa zoezi la upigaji dawa majumbani ili tuendelee kuupiga vita ugonjwa wa malaria hapa nchini.

58. **Mheshimiwa Spika,** Tutaendelea kuhakikisha tunaimarisha zaidi huduma za matibabu, upatikanaji, utunzaji na usambazaji wa dawa, huduma za mpango wa damu salama, huduma za udhibiti wa kemikali, chakula, dawa na vipodozi. Aidha, tutahakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa vya tiba; ununuzi wa vitendanishi vya vinasaba (DNA) pamoja na vifaa vya maabara unakuwa endelevu sambamba na kuongeza idadi ya rasilimali watu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kila inapohitajika.

59. **Mheshimiwa Spika,** nitoe wito kwa wanajamii wenzangu tuendelee kutumia huduma zinazotolewa na hospitali zetu zilizomo katika wilaya zetu na inapobidi katika hospital za rufaa. Vilevile, niendelee kuwakumbusha kuendelea kuchukua tahadhari za kujikinga na maradhi yasiyoambukiza na ya mripuko ambayo yamekuwa yakiibuka siku hadi siku yakiwemo saratani ya matiti, kisukari, shindikizo la damu na ulinganisho wa uzito na kimo cha mwili (BMI) pamoja na kujikinga na maradhi ya miripuko kama vile kipindupindu na COVID - 19 kwa kufuata miongozo ya wataalamu wetu wa afya.

**Sekta ya Elimu**

60. **Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu tarehe 23 Septemba 1964 Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Kwanza wa Baraza la Mapinduzi alitangaza elimu bila malipo kwa Wazanzibari wote. Hali ambayo imepelekea kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji wa watoto, kuimarika kwa miundombinu ya elimu pamoja na kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi. Mafanikio haya yametokana na jitihada na mkazo wa Serikali katika kuinua ubora wa elimu hapa nchini. Napenda kuwahakikishia kuwa tutaendelea kuyasimamia mafanikio haya kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa elimu wakiwemo wazazi, wanafunzi, washirika wa maendeleo wa ndani na nje pamoja na sekta binafsi.

61. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa skuli mbili katika maeneo ya Mwanakwerekwe kwa Unguja na Wingwi kwa Pemba. Aidha, ujenzi wa vituo 22 vya

ubunifu wa Kisayansi vinavyojumuisha maabara, maktaba na madarasa 48 katika skuli mbalimbali za Unguja na Pemba nao umekamilika. Na hivi sasa tayari wanafunzi wameanza kutumia miundombinu hii kwa kuendelea na masomo yao. Kwa kuzingatia umuhimu wa elimu, Serikali bado inaendelea na mipango yake ya kujenga skuli, kukamilisha ujenzi wa Madarasa 300 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi (200 Msingi na 100 Sekondari), kuwapatia wanafunzi 106,625 vikalio, kujenga maabara na maktaba katika skuli 11 za Sekondari, kuandaa na kuimarisha matumizi ya TEHAMA na Media katika kujifunza (Virtual Learning Environment) pamoja na kuendelea kufanya tafiti zenye ajenda za maendeleo ya kiuchumi ikiwemo Uchumi wa Buluu kupitia wataalamu wake wa Chuo kikuu cha Taifa SUZA. Napenda kuchukua fursa hii kuwahimiza wadau wote wa elimu kushirikiana na Serikali katika kuinua zaidi kiwango cha elimu na hatimae kuwa na wataalamu wazalendo kwa manufaa ya nchi yetu na dunia kwa ujumla.

**Kukabiliana na Maafa**

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kukabiliana na maafa imeendelea kuijengea uwezo jamii juu ya kukabiliana na maafa mbali mbali yanayoweza kutokea. Tunafahamu kuwa moja kati ya changamoto kubwa ya athari za kimaafa zinazoikumba nchi yetu ni athari za mvua kubwa zinazotokea maeneo mbali mbali ya visiwa vya Unguja na Pemba. Nachukua fursa hii kuwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari juu ya athari zinazosababishwa na mvua hizo ikiwemo mafuriko au kuanguka kwa miti na majengo. Ni vyema vilevile tukazingatia na kufuata sheria na kanuni za mipango miji na vijiji, mazingira na afya ya jamii katika kutafuta maeneo ya kuishi na utaratibu wa ujenzi katika maeneo hayo. Vilevile, tuendelee na utaratibu wa kusafisha mazingira yetu yanayotuzunguka ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza.

63. **Mheshimiwa Spika,** Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiepusha nchi yetu dhidi ya majanga mbalimbali yanayoikumba dunia. Mwenyezi Mungu ametuepusha na tishio la janga la hivi karibuni la

kimbunga kinachojulikana kwa jina la "Jobo". Nawaomba wananchi wote tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu azidi kuiweka nchi yetu katika hali ya salama muda wote.

**Vitendo vya Ukatili wa Kijinsia na Udhalilishaji**

64. **Mheshimiwa Spika,** licha ya jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji kwa makundi mbalimbali ya kijamii, bado vitendo hivi vinaendelea kukithiri katika nchi yetu. Kwa mujibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali na Jeshi la Polisi hapa Zanzibar, kwa mwaka 2020 pekee kumeripotiwa jumla ya matukio 1,363 (217 na watoto 1,146) yanayohusiana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto. Aidha, katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita (Januari – Machi 2021) matukio 362 (wanawake 48 na watoto 315) tayari yameripotiwa. Kwa kweli hii ni idadi kubwa mno kuishuhudia ikiwa inatokea katika nchi yetu.

65. **Mheshimiwa Spika,** hali hii inaonesha wazi kuwa bado Serikali ina kazi kubwa ya kufanya katika kudhibiti vitendo hivyo viovu katika jamii yetu. Bila shaka wafanyaji wa vitendo hivi wamo katika jamii zetu, tunawajua, tunaishi nao na tunazungumza nao; lakini ama tunawaficha au tunayaficha matendo wanayoyafanya kwa sababu ya muhali tulio nao. Wito wangu kwa wananchi, kitendo cha kumficha muhalifu manaake ni kuwa unashirikiana nae katika uhalifu huo; hivyo tuache kabisa kuoneana muhali katika kuripoti vitendo hivi viovu katika jamii zetu. Aidha, Viongozi katika Shehia, Wilaya na Mkoa, tukumbuke moja ya majukumu yetu muhimu ni kupunguza au kuondosha kabisa vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto katika maeneo yetu.

66. **Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa Wilaya ya Mjini ndiyo inaongoza kwa kiasi kikubwa kuwa na matukio hayo ikifuatiwa na Wilaya za Magharibi A na B. Hii inaonesha kuwa wanahitaji kuweka nguvu zaidi katika kuweka mikakati ya kupambana na vitendo hivyo sambamba na kuchukua hatua kwa wale watakaobainika kusababisha na kufanya vitendo hivyo.

67. **Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kuchukua kila aina ya jitihada kuhakikisha wimbi hili ya udhalilishaji katika nchi yetu linapungua na kumalizika kabisa. Tuatendelea kutengeneza mikakati ya kimawasiliano ili kuleta mabadiliko ya tabia kwa jamii na kuihamasihsa jamii kuongeza kasi ya kupambana na vitendo hivi kwa kutumia njia mbali mbali ikiwemo mikutano mihadhara na vyombo vya habari, kuyawezesha mabaraza ya watoto ya Shehia na Vilabu vya skuli kujitambua na kuripoti matukio kama haya.

68. **Mheshimiwa Spika,** Serikali tayari imeanzisha Mahakama maalum ya kushugulikia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia kama ilivyoelekezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi. Tayari Mahakama hizo zimeshaanza kazi na Mahakimu wameshapangiwa vituo vyao kwa Unguja na Pemba na hadi mwezi wa Aprili 2021 takwimu zinaonesha kuwa jumla ya kesi 180 zimeshafunguliwa. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa agizo lake hili ambao tayari limeshafanyiwa kazi. Ni imani yangu kuwa Mahakama hii itatoa mchango mkubwa katika kushughulikia kesi za aina hiyo na hatimae kupunguza au kuondosha kabisa vitendo hivyo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya watoto na Wanawake hapa nchini.

**Mapambano dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi**

69. **Mheshimiwa Spika,** miongoni mwa mambo makubwa yanayorejesha nyuma jitihada za Serikali na wananchi katika kufikia maendeleo ni vitendo vya rushwa. Vitendo vya rushwa vikienea katika nchi basi utoaji wa huduma kwa wananchi unakuwa hafifu na unanyima haki ya kuhudumiwa hasa kwa wanyonge. Bado kuna viongozi na watendaji wa Serikali ambao hawatoi huduma mpaka wapewe fedha au kitu chochote kutoka kwa anaetarajiwa kupokea huduma. Huu ni utumiaji mbaya wa madaraka au nafasi ambayo mtu amepewa na Serikali.

70. **Mheshimiwa Spika,** kuna tuhuma nyingi za makosa ya rushwa na uhujumu uchumi ikiwemo, kuomba rushwa, matumizi mabaya ya ofisi na mali za Serikali, utakasishaji fedha na mgongano wa maslahi ambazo

zinaendelea kushughulikiwa na chombo chetu cha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Kuhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA). Kuna miradi mingi imetekelezwa ambayo imetumia fedha nyingi ambazo haziendani na thamani ya matokeo ya miradi hiyo. Mamlaka hii itaendelea kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha mchakato wake na utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo imejidhatiti kufuata misingi ya utawala bora itaendelea kuchukua hatua madhubuti za kupambana na vitendo vya namna hiyo ambavyo kimsingi vinaipaka matope Serikali yetu.

71. **Mheshimiwa Spika,** suala la utawala bora linakwenda sambamba na uwajibikaji. Nachukua nafasi hii kuwataka viongozi wenzangu na watendaji wote wa Serikali kuzingatia sana jukumu letu la kutoa huduma bora kwa wananchi. Kila mmoja ahakikishe anafanyakazi zake kama alivyoelekezwa na taasisi au Mamlaka iliyomueka sehemu aliopo. Bila kuwajibika maendeleo kwetu itakuwa ni ndoto. Nchi zote zilizopata maendeleo ni kwa juhudi kubwa zilizochukuliwa na viongozi, watendaji na wananchi katika kutumia rasilimali zao kwa kufuata miongozo na taratibu walizojiwekea wenyewe. Hakuna nchi iliyoendelea kwa kutegemea misaada na rasilimali za nje. Hivyo, viongozi ni lazima kuwa mfano kwa watendaji wao na wananchi kwa jumla katika uwajibikaji na uzalendo. Kwa kufanya hivyo tutakuwa kweli tunamuunga mkono na kumsaidia kwa dhati Rais wetu katika kufikia azma ya Serikali hii ya Awamu ya Nane ya kuleta neema kwa wananchi.

72. **Mheshimiwa Spika,** kasi yetu ya kuwaletea maendeleo wananchi na nchi kwa jumla inategemea namna tunavyowajibika kwa pamoja. Hivyo, Serikali haitomvumilia yeyote atakaejaribu kurejesha nyuma jitihada zetu, itabidi tumuache au yeye atuache; sisi tuendelee. Serikali kwa upande wake itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha hali ya utendaji ikiwemo maslahi na mazingira ya kufanyia kazi kwa wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wa hali ya juu.

**Suala la Migogoro ya Ardhi**

73. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea na kushughulikia suala la uimarishaji wa matumizi ya ardhi kwa kuchukua hatua mbalimbali ili kuwa na usawa wa matumizi kwa wananchi wote. Katika kusimamia haki za wananchi kwenye matumizi ya ardhi, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ametenga siku maalum kila wiki kukutana na wananchi wenye migogoro ya ardhi pamoja na wapangaji wa Shirika la Nyumba ili kusikiliza malalamiko yao na kwa pamoja kuyatafutia ufumbuzi unaostahiki bila ya migongano. Hatua hii inakwenda sambamba na kufanya ziara za mara kwa mara katika maeneo hasa yanayoripotiwa zaidi kukithiri kwa migogoro. Hadi sasa jumla ya migogoro 99 imeshasikilizwa ambapo migogoro 61 ipo katika hatua ya kutatuliwa na migogoro 38 imetolewa maelekezo ya awali kwa ajili ya ufuatiliaji. Aidha, wizara imeunda kamati ya wataalamu ya ufuatiliaji wa migogoro ya ardhi inayojumuisha wanasheria wa Wizara, Wapimaji Ardhi na Maafisa Mipango inayoripoti kwa Katibu Mkuu kila wiki kwa ajili ya mashauriano na utatuzi wa pamoja.

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa migogoro inayowasilishwa Mahakama ya Ardhi, hadi sasa Mahkama imeshapokea kesi 3,603 ambapo kesi zilizomalizika ni 3,384 na kesi 219 zinaendelea. Pia, kupitia mtandao wa Sema na Rais Mwinyi (SNRMWINYI) Wizara imeshapokea malalamiko 77 ambapo malalamiko manane (8) yameshatatuliwa na 69 yanaendelea kufuatiliwa kwa ukaribu zaidi. Hata hivyo, licha ya kuwapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya, naomba kutoa wito kwa Viongozi na watendaji wa sekta hii pamoja na wale wa Shirika la Nyumba kuongeza kasi ya kuitafutia ufumbuzi migogoro yote ya ardhi iliyopo lakini pia kuacha tabia ya kusababisha migogoro hiyo kutokana na vitendo vya baadhi yao kujiingiza katika biashara ya kuuza ardhi au viwanja.

75. **Mheshimiwa Spika,** Inasikitisha kuona kwamba bado kumekuwa na idadi kubwa ya malalamiko yanayohusiana na migogoro ya ardhi katika Afisi zetu za Wakuu wa Mikoa na Wilaya. Kwa kipindi cha Julai

hadi Machi 2020/2021, Afisi hizo zimepokea malalamiko takriban 500 ambayo mengi yao yahusiana na uvamizi wa maeneo, matumizi ya eka tatu, mipaka ya mashamba na viwanja pamoja na umiliki na matumizi ya ardhi ambapo baadhi ya maeneo yanawamiliki wenye hati zaidi ya mtu mmoja. Tunaendelea kuwasisitiza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kufuatilia kwa karibu migogoro ya ardhi katika maeneo yao na kusuluhisha huku wakizingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Na iwapo watagundua kuwa kuna baadhi ya watendaji au viongozi wamehusika na migogoro hiyo kwa tamaa zao basi wasisite kuwachukulia hatua kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo. Na sisi viongozi wa juu kwa upande wetu hatutomvumilia kiongozi au mtendaji yeyote atakaebainika kuhusika kwa njia yeyote katika kusababisha migogoro hiyo.

76. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha huduma za mawasiliano baina ya serikali na wananchi Serikali imeanzisha Mfumo Maalum wa Mawasiliano unaojulikana kwa jina la Sema na Rais Mwinyi (SNRMWINYI) uliozinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk Hussein Ali Mwinyi. Mfumo huu unawezesha kuzifahamu changamoto za kiutendaji kwa haraka na kuweza kuzishughulikia na kutatua kero za wananchi kwa haraka kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma zinazohitajika. Tayari mfumo huu umeanza kuleta matokeo chanya kwani kero nyingi za wananchi zimeweza kutatuliwa kupitia Idara, taasisi na mamlaka nyengine za Serikali zinazohusika. Nitoe wito kwa wananchi kuutumia mfumo huu kwa uaminifu ili kuongeza kasi ya utoaji wake wa huduma kwa kila anaehitaji.

**Uratibu wa Sera**

77. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki cha Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kuratibu Sera za Serikali. Uamuzi huu umechukuliwa makusudi ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na utaratibu mzuri wa utungaji sera za kitaifa na zile za kisekta pamoja na kuhakikisha kuwa zinakidhi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Tayari, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi imeanza kuzichambua Sera za Kisekta 35 zilizopo hapa nchini kwa kuzioanisha na Mipango Mikuu ya Maendeleo ya Nchi, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na Miongozo ya Kikanda na Kimataifa ambayo imeridhiwa na nchi yetu.

78. **Mheshimiwa Spika,** tunaamini kuwa shughuli za uratibu wa Sera ambao utahusisha pia kutoa maelekezo na kufuatilia utekelezaji wa Sera hizo kwa kila atakaehusika kutaleta mabadiliko makubwa katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Wito wangu kwa taasisi na sekta kutoa mashirikiano yao yote kwa timu zitakazohusika na kazi hiyo ili kwa pamoja tulifikie lengo letu.

**Suala la Ugatuzi**

79. **Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya maamuzi ya kurudisha sekta zilizogatuliwa kwa Wizara husika. Uamuzi huo wa serikali umezingatia zaidi changamoto ambazo zilijitokeza wakati wa utoaji huduma, pamoja na kupata maoni ya wadau hasa wapokea huduma na watumishi wa umma wanaotekeleza Mfumo wa Ugatuzi. Makabidhiano rasmi ya sekta hizo ambazo ni Kilimo, Afya na Elimu kurudi katika Wizara zao yanatarajiwa kufanyika mwezi Julai 2021.

80. **Mheshimiwa Spika,** bila shaka uamuzi wa kuzifanya sekta hizo kwenda kwenye mfumo wa ugatuzi hapo awali ulitokana na changamoto zilizokuwa zikijitokeza. Kutokana na uchunguzi uliofanyika, changamoto hizo nyingi zimeendelea kuwepo na nyengine zimeongezeka. Hivyo, Serikali imeamua kuzirejesha sekta hizo katika Wizara zao "mama" na itahakikisha kuwa changamoto zilizokuwepo awali zinaondoshwa kabisa. Nachukua nafasi hii kuwahakikishia wananchi kuwa utoaji wa huduma katika Afisi zetu za Serikali za Mitaa ambazo ni Mabaraza ya Miji, Manispaa na Halmashauri za Wilaya utaendelea kama kawaida. Afisi hizi zitaendelea kusimamia mambo ya msingi ikiwemo usafi wa Miji na kutoa tozo stahiki kwa wafanyabiashara kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao kwa kushirikiana na sekta husika.

## UTEKELEZAJI WA KAZI ZA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI - MACHI 2020/2021

81. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za kawaida na miradi ya maendeleo kwa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi zinatekelezwa kupitia Idara saba, Taasisi tatu pamoja na Vitengo sita vinavyoripoti moja kwa moja kwa Katibu Mkuu. Kutokana na utaratibu wa Serikali wa kutekeleza majukumu yake kwa kutumia Bajeti inayotumia Programu (Programme Based Budget), Afisi kupitia Idara na Taasisi hizo inatekeleza Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14.

## AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS (C01)

### PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS

1. ***Programu Ndogo (SC010101) : Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais***

82. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina Programu Ndogo moja ya Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais. Jukumu lake ni kuratibu shughuli za Makamu wa Pili wa Rais pamoja na utoaji wa huduma zote muhimu kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeratibu ziara 110 za ndani za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais za ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika taasisi, wilaya na mikoa ikiwemo kukagua miradi na kufuatilia shughuli za kimaendeleo;

ii. Imeratibu vikao 16 baina ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na wageni mbalimbali wakiwemo Mabalozi na Wageni Mashuhuri ili kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kibiashara baina ya Zanzibar na nchi au mashirika wanayotoka Wageni hao.

iii. Imeratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi alizozitoa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kwa wananchi, taasisi na jamii zikiwemo kuchangia ujenzi wa Hospitali ya Kidagoni, ununuzi wa vifaa vya michezo kwa ajili ya vijana na bati kwa

ajili ya uwezekaji wa Tawi la CCM Chonja Micheweni, ununuzi wa tangi kubwa la maji Meli Nne pamoja na ununuzi wa Jokofu katika soko la Samaki Njuguni, Micheweni.

iv. Imefanya matengenezo makubwa na madogo katika nyumba ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais iliopo Mazizini;

v. Imetoa taarifa za matukio yote aliyofanya na kushiriki Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais sambamba na kuhifadhi jumla ya matukio 65, hotuba 21 na Picha 770 kwa ajili ya kumbukumbu na matumizi ya baadae.

vi. Afisi imeendelea kushughulikia malalamiko, migogoro na kero mbali mbali za wananchi ambapo jumla ya malalamiko 108 yamepokelewa na malalamiko 79 sawa asilimia 73 tayari yamepatiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika. Afisi inaendelea kufuatilia hatua zinazochukuliwa katika kuyapatia ufumbuzi malalamiko yaliyobakia yaliopo katika Taasisi mbali mbali za Serikali na Binafsi.

83. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii Ndogo iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 1,443,495,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni **Shilingi 900,844,423** ambazo ni sawa na **asilimia 62** na **asilimia 120** kwa fedha zilizopangwa miezi tisa

## PROGRAMU KUU - (PCO102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

84. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuweka mfumo imara na endelevu wa utoaji na upatikanaji wa huduma bora za Serikali kwa jamii kupitia Programu Ndogo nne ambazo ni Kukabiliana na Maafa, Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa, Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli za SMZ Dodoma.

***Programu Ndogo – SCO10201: Kukabiliana na Maafa***

85. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina jukumu la kuainisha, kuimarisha na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Kukabiliana na Maafa hapa Zanzibar. Katika kipindi cha miezi tisa kwa 2020/2021, Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Imeratibu utoaji wa huduma katika matukio ya majanga yaliyotokea Unguja na Pemba yakiwemo matukio 45 ya ajali za moto, ajali nne za baharini, matukio 13 ya upepo mkali pamoja na tukio la mafuriko lililoathiri jumla ya nyumba 14 katika Wilaya ya Kusini. Vilevile, Ofisi imeratibu shughuli za uokozi na utoaji wa huduma katika tukio la kuporomoka kwa jengo la Beit el Ajab liliopo Forodhani na kusababisha vifo vya watu wawili (2) na watu wanne (4) kujeruhiwa;

ii. Imeifanyia matengenezo mitambo ya redio ya HF na VHF katika vituo vya Makunduchi, Gamba, Maruhubi kwa Unguja na Chakechake kwa upande wa Pemba. Mitambo hiyo hivi sasa inafanyakazi kwa ukamilifu wake;

iii. Afisi kupitia Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa imetoa tahadhari kwa jamii juu ya muelekeo wa mvua za vuli za mwaka 2020 na Masika 2021 kupitia ZBC redio na televisheni na mitandao ya kijamii ili wananchi kuchukua hatua stahiki za kujiandaa;

iv. Imetoa tahadhari juu ya muelekeo wa mvua za vuli za mwaka 2020 na Mvua za Masika zilizoanza kunyesha mwishoni mwa mwezi wa Februari, 2021 pamoja na kupanga mikakati ya kufuata katika kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza. Vilevile, katika kipindi hiki shughuli hiyo imefanyika maalum katika Shehia 37 zilizopo maeneo hatarishi ya kukumbwa na mafuriko Unguja;

v. Imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa makundi mbalimbali ya jamii wakiwemo viongozi wa kidini 30, wenyeviti

wa kamati za maafa za Shehia 127 pamoja na wanafunzi 1,927 kutoka skuli 10 zenye dakhalia Unguja na Pemba zikiwemo Utaani, Chasasa na Chuo cha Kiislamu; wafanyakazi 15 kutoka taasisi moja isiyo ya Kiserikali na masheha 129 kisiwani Pemba;

vi. Imefanya ukaguzi katika maeneo 15 yakiwemo maghala ya kuhifadhia vyakula, skuli, Mkokotoni eneo la fungu refu, eneo la Mtoni Kidatu pamoja na maeneo ya miundombinu ya barabara ili kubaini changamoto zilizopo katika kukabiliana na maafa na kuzipatia ufumbuzi;

vii. Imefuatilia na kufanya tathmini ya shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati za Maafa za Wilaya ili kubaini mafanikio na changamoto zinazowakabili;

viii. Imefanya kikao kimoja cha Kamati ya Kitaalamu ya Kukabiliana na Maafa ambacho kilijadili hali ya maradhi ya homa kali ya mafua na kupumua na hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika kujikinga na maradhi hayo;

ix. Imesimamia umalizaji wa ujenzi wa vijiji vya wananchi walioathiriwa na Mvua za Masika za mwaka 2017 vilivyojengwa Nungwi na Tumbe pamoja na kuratibu shughuli ya makabidhiano ya vijiji hivyo baina ya Taasisi ya Mwezi Mwekundu ya Falme za Kiarabu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyofanyika Nungwi tarehe 01 Machi, 2021; Sambamba na kufanya tathmini ya familia 60 zinazotarajiwa kupatiwa nyumba hizo za makaazi na kulipa fidia kwa wananchi 18 walioathiriwa na mradi huo kwa eneo la Tumbe Pemba;

**86.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii Ndogo iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 1,086,826,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni **Shilingi 537,633,405** ambazo ni sawa na **asilimia 49** na **asilimia 65** fedha zilizopangwa miezi tisa. Aidha, Programu hii Ndogo ilipanga kutumia

**Shilingi 186,000,000** kwa kazi za maendeleo na hadi Machi 2021 ilipata **Shilingi 186,000,000** ambazo ni sawa na asilimia 100.

***Programu Ndogo – SCO10202: Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa***

87. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Miongoni mwa Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa yanayoratibiwa na Programu hii ni Sherehe za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari, 1964, Maadhimisho ya Siku ya Kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na ushiriki wa viongozi na wananchi wa Zanzibar katika Sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara. Aidha, Programu hii inaratibu mazishi ya viongozi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa Nam. 5 ya Mwaka 2019.

88. **Mheshimiwa Spika,** Progrmu hii ndogo ambayo inatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2020 – Machi 2021, imetekeleza shughuli zifuatazo:-

    i. Imeratibu na kusimamia maadhimisho ya Sherehe za Miaka 57 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ambayo kilele chake kilifanyika tarehe 12 Januari, 2021 katika Viwanja vya Mnazi Mmoja na mgeni rasmi alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Husein Ali Mwinyi;

    ii. Ofisi imeratibu Maadhimisho ya Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa kwa kuzuru na kuwaombea dua viongozi Wakuu wa Kitaifa waliotangulia mbele ya haki ambao ni Marehemu Sheikh Idriss Abdul Wakil, Marehemu Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi, Marehemu Dkt. Omar Ali Juma, Marehemu Brg. Gen. Mstaafu Ramadhan Haji Faki na Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad. Aidha, Afisi imeratibu Siku ya Kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume kwa kusoma Hitima na Dua katika Afisi Kuu ya CCM, Kisiwandui tarehe 7 Aprili, 2021;

iii. Imeratibu na kushiriki katika sherehe za kumuapisha Rais Mteule wa Awamu ya Nane wa Zanzibar Mheshimiwa Dk Hussen Ali Mwinyi, sherehe iliyofanyika Uwanja wa Amaan Zanzibar. Aidha, imeshiriki katika uratibu wa sherehe za kumuapisha aliyekuwa Rais Mteule wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, sherehe zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri Mkoani Dodoma ambapo viongozi wa Serikali na wananchi 100 kutoka Zanzibar walishiriki;

iv. Imeshiriki katika kuratibu mazishi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Benjamin William Mkapa ambae amezikwa tarehe 29/07/2020 kijijini kwao Lupaso – Mtwara;

v. Imeratibu mazishi ya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad aliefariki tarehe 17/02/2021 na kuzikwa tarehe 18/02/2021 kijijini kwao Mtambwe – Nyali Pemba; Aidha, Imeratibu dua/hitma iliyofanyika tarehe 19/02/2021 Uwanja wa Jadida Wete Pemba na 20/02/2021 Uwanja wa Maisara mjini Unguja;

vi. Imeratibu ushiriki wa Viongozi na Wananchi katika kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika vituo vya Dar es salaam na Zanzibar. Aidha, imeratibu ushiriki wa Viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mazishi ya Kiongozi huyo yaliyofanyika siku ya tarehe 26/03/2021 kijijini kwao Chato Mkoa wa Geita;

vii. Tumelijengea kaburi la aliyekuwa Waziri Kiongozi Mstaafu Marehemu Brg. Gen. Mstaafu Ramadhani Haji Faki lililoko Mkwajuni Unguja na kaburi la aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad lililoko Mtambwe Pemba;

**89. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii Ndogo iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 1,270,817,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni **Shilingi 498,304,293** ambazo ni sawa na **asilimia 39** na **asilimia 41** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa.

***Programu Ndogo – SCO10203: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar***

**90. Mheshimiwa Spika,** Program Ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ina jukumu la kuratibu shughuli za SMZ, masuala ya Muungano, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, Utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali katika kipindi cha miezi tisa (Julai 2020 – Machi 2021), imetekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Imeratibu kikao cha Awali cha Mawaziri na Makatibu Wakuu kuhusu Masuala ya Muungano, kilichofanyika Dar-es Salaam tarehe 16 Oktoba 2020;

ii. Imeratibu na kushiriki hafla ya kusainiwa kwa Hoja tano za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi. Hafla hiyo iliyofanyika tarehe 17 Oktoba 2020 Ikulu Dar es Salaam ilikuwa chini ya uenyekiti wa aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Hoja hizo ni Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia; Ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda; Gharama za Kushusha Mizigo (Landing Fees); na Utaratibu wa Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano;

iii. Imeratibu na kusaidia ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya Wabunge kwa mwaka wa

fedha 2016 – 2019 kwa upande wa Zanzibar ikihusisha pia majibu ya Hoja za Ukaguzi wa Mfuko huo kwa kipindi hicho;

iv. Imeandaa na kuchapisha nakala za taarifa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 – 2020 kwa kipindi cha miaka mitano na kuwasilisha katika kikao cha Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Dodoma;

v. Imeandaa taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2020 – 2025 kwa kipindi cha nusu mwaka Oktoba 2020 – Machi, 2021;

vi. Kuandaa na kushiriki ziara za kikazi kwa taasisi za Muungano na zisizo za Muungano kwa ajili ya kujifunza na kubadilishana uzoefu katika utendaji kazi wa taasisi hizo kwa manufaa ya pande zote mbili;

vii. Imefanya vikao vitatu vya kisekta vya utafiti pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) na Idara ya Utafiti ya Tume ya Mipango ambapo orodha ya watafiti wote waliofanya utafiti Zanzibar kuanzia mwaka 2010 - 2020 imetolewa kwa ajili ya kufuatiliwa ili taarifa za tafiti zao zitumike ipasavyo. Aidha, kikao cha pamoja na ZAHRI kilitoa muafaka wa changamoto zinazowakumba watafiti katika sekta ya Afya;

viii. Imeratibu na kusimamia utoaji wa vibali 361 vya utafiti kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi ili kuwawezesha kufanya tafiti katika maeneo ya Zanzibar;

ix. Inaendelea na kazi ya awali ya kukusanya na kuzipitia Sera zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuangalia uandaaji wa sera hizo, mafanikio ya utekelezaji na mapungufu yaliyojitokeza;

x. Imeendelea kutoa taarifa za shughuli mbali mbali zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika mitandao ya kijamii ikiwemo facebook, instagram na twitter;

xi. Imefanya na kusimamia awamu mbili za uhakiki wa walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini ambapo hadi sasa jumla ya Kaya 27,495 kati ya Kaya 32,077 zimehakikiwa sawa na asilimia 85.7 ya walengwa wote Unguja na Pemba ili kujiridhisha na kuondoa Walengwa wasio na sifa;

xii. Imekusanya orodha ya walengwa wapya wa Mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF III) Awamu ya Pili katika shehia zote 388 (Unguja 159 na Pemba 129) ambao hawakuwemo katika mpango wa TASAF III Awamu ya Kwanza;

xiii. Imesimamia uhaulishaji wa fedha kwa Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa kipindi cha Julai hadi Machi kwa walengwa wa kaya maskini Unguja na Pemba ambapo jumla ya **Shilingi 2,891,934,000** zililipwa baada ya Uhakiki uliofanywa kwa Walengwa 27,020 (14,866 Unguja 12,154 Pemba);

xiv. Imeendelea kusimamia Mradi wa ujenzi wa madarasa matatu katika skuli ya Sekondari Mahonda; Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Utawala Skuli ya Sekondari Mahonda; na Mradi wa Ujenzi wa Ukumbi wa Mitihani Skuli ya Sekondari Fujoni. Hatua ya ujenzi katika miradi yote imefikia **asilimia 98;**

xv. Imetoa elimu kwa Mamlaka ya Utekelezaji wa TASAF ya Pemba na kuwahusisha Masheha na Walengwa 940 juu ya matumizi ya taasisi za kifedha kwa kuviendeleza vikundi vyao vya kuweka akiba na kukuza uchumi wa Kaya. Aidha, Mafunzo juu ya uibuaji wa Miradi ya kutoa ajira za muda yametolewa kwa Wawezeshaji 104 wa Unguja na Pemba. Mafunzo hayo, yatawawezesha Wawezeshaji hao kuibua na kusimamia miradi ya aina hiyo;

xvi. Imeendesha kikao cha Kamati ya Uongozi wa TASAF Unguja ambacho kilipitisha na kuidhinisha maombi ya fedha **Shilingi 6,806,267,150** kwa kaya 16,239 za ruzuku ya uzalishaji (Productive grants);

xvii. Imetoa mafunzo na elimu kwa Wajumbe wote wapya wa Baraza la Wawakilishi kuhusu Sheria Nambari 4 ya mwaka 2012 ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ili kuwawezesha Waheshimiwa kufuata na kutekeleza shughuli za Mfuko kwa mujibu wa Sheria. Aidha, ofisi imewakumbusha na kuwataka Waheshimiwa Wawakilishi kuandaa wajumbe wapya wa Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa mujibu wa matakwa ya Sheria husika;

xviii. Imefuatilia uendeshaji na utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa majimbo 50 ya Zanzibar na kuratibu utatuzi wa changamoto zinazojitokeza katika uendeshaji wa Mfuko katika majimbo;

xix. Imeratibu na kusimamia uingizwaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wa Wabunge kwa mwaka 2020/2021;

xx. Imeratibu vikao vinane vya ushirikiano baina ya Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) ambazo ni:-

a. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (SMZ) na Afisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira (SMT);

b. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (SMZ) na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi (SMT);

c. Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi (SMZ) na Afisi ya Waziri Mkuu – Sera, Uratibu wa Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu (SMT);

d. Wizara ya Maji na Nishati (SMZ) na Wizara ya Maji (SMT);

e. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ) na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SMT);

f. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (SMT) na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi (SMZ);

g. Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo (SMZ) na Wizara ya Kilimo (SMT); na

h. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo (SMZ) na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (SMT).

xxi. Imeratibu na kushiriki katika maandalizi ya vikao vya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC). Vikao hivyo ambavyo vilifanyika kwa njia ya Video (Virtual meeting) vilihusisha Watendaji na Maofisa Waandamizi (tarehe 4 – 7 Machi, 2021), Makatibu Wakuu (tarehe 8-11 Machi, 2021) na Mawaziri tarehe (12 – 13 Machi, 2021). Kwa upande wa Tanzania vikao vilifanyika katika vituo vya Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam na Ukumbi wa Mikutano wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB);

xxii. Imeratibu na kushiriki kazi za Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kufuatilia Hesabu za Serikali (PAC) kwa Unguja na Pemba juu ya Hoja za ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kwa mwaka 2016 – 2018, ambapo Kamati hiyo ilipata majibu ya hoja mbalimbali zilizoibuliwa;

**91. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii Ndogo iliidhinishiwa kutumia **Shilingi 750,757,000** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni **Shilingi 443,814,163** ambazo ni sawa na asilimia 59 na asilimia 83 kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa. Aidha, Programu hii Ndogo ilipanga kutumia **Shilingi 21,597,995,000** kwa kazi za maendeleo na hadi Machi 2021 ilipata **Shilingi 1,032,500,000** ambazo ni sawa na asilimia 5. Vilevile Baraza hili liliidhinisha matumizi ya **Shilingi 14,100,000,000** ikiwa ni ruzuku

kwa Idara ya Uhamiaji, Zanzibar na hadi Machi 2021 ilipata **Shilingi 2,395,000,000** ambazo ni sawa na asilimia 17 au **asilimia 23** kwa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa.

**Programu Ndogo – SCO10204: Shughuli za SMZ Dodoma**

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Shughuli za SMZ Dodoma jukumu lake kuu ni kuratibu shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Tanzania Bara yenye lengo kukuza na kuimarisha ushirikiano baina SMZ na Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Kimataifa na Ofisi za Kibalozi. Kazi zilizotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

i. Imeratibu ziara ya aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad kwenda kufunga maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam tarehe 9 Disemba 2020;

ii. Imeratibu ziara ya kimafunzo ya Kampuni ya Ujenzi ya SMZ kutembelea Taasisi tatu ambazo ni Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), Jeshi la Magereza, na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) Dar es Salaam na Dodoma, sambamba na ziara ya Ofisi ya Wakala wa Majengo Zanzibar kukutana na uongozi wa TBA Dar es Salaam, Ofisi ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma na kwenda kuangalia kiwanja cha SMZ Dodoma;

iii. Imeratibu ziara ya maofisa wa ZBC kutembelea kituo cha TV cha Azam, TBC na Channel 10;

iv. Afisi imeratibu upatikanaji wa VISA 12 kwa ajili ya safari za nje kwa viongozi mbalimbali wa Serikali;

v. Afisi inaendelea na hatua za kufanya utafiti wa kutathmini huduma zinazotolewa na Ofisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma

ambapo tayari 'Concept Note' imekwishaandaliwa na sasa utafiti unaendelea kukusanya taarifa husika kwa wadau wa upande wa Zanzibar;

vi. Afisi imewapatia mafunzo maafisa wake juu ya masuala ya Itifaki tarehe 30 Disemba, 2020 yaliyofanywa na mkufunzi kutoka Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini Dar es Salaam;

vii. Imeratibu na kushiriki vikao 13 vya mashirikiano ya kazi baina ya Wizara za SMZ na SMT; vikao viwili vya Taasisi na Jumuiya za Kimataifa ambazo ni Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Aidha, imeshiriki vikao sita vya Kibalozi:- Sweden, Saud Arabia, Denmak, Ujerumani, Japan na Canada.

93. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii Ndogo iliidhinishiwa kutumia Shilingi 669,852,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni Shilingi 403,137,351 ambazo ni sawa na asilimia 60 na asilimia 77 kwa fedha zilizopangwa kutumika kwa miezi tisa.

**PROGRAMU KUU - (PCO104): UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

94. **Mheshimiwa Spika,** Programu Kuu hii ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi inahusika na uimarishaji wa mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za kiofisi za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi. Programu hii ina Programu Ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Afisi Kuu Pemba.

***Programu Ndogo – CO10401: Uongozi na Utawala***

95. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji na inahusika na usimamizi wa rasilimali watu

na utekelezaji wa kazi za kila siku za Afisi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2020/2021 Programu ndogo hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeendelea kusimamia maslahi na kuwapatiwa wafanyakazi stahiki zao zikiwemo za mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF), likizo la kawaida na posho la likizo kwa wanaostahiki, malipo baada ya saa za kazi na kutoa ubani kwa wafiwa. Vilevile, wafanyakazi 25 walirekebishiwa mishahara yao na kupangwa katika madaraja baada ya kurejea masomoni na wafanyakazi wanne (4) wametayarishiwa mafao yao ya kustaafu na kuwasilishwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa hatua ***(Angalia Kiambatanisho Nam. 1);***

ii. Afisi imewaendeleza wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi ili kuwajengea uwezo kitaaluma katika kada tofauti kwa mujibu wa mahitaji, ambapo jumla ya wafanyakazi 62 wamepatiwa mafunzo ya muda marefu. Aidha, semina mbalimbali zimetolewa kwa wafanyakazi 187 wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ili kuongeza uelewa wa kusimamia na kutekeleza Sheria za Utumishi wa Umma na kinga juu ya maradhi ya UKIMWI; na wafanyakazi 272 wamepatiwa mafunzo ya athari za rushwa na uhujumu uchumi. Vile vile, wafanyakazi 26 wamepatiwa mafunzo ya awali ambapo 22 kati yao wamethibitishwa kazini. ***Angalia Kiambatanisho 2 na 3;***

iii. Afisi imeendesha kikao kimoja cha Kamati ya Uongozi na vikao vinane (8) vya Kamati Tendaji kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

iv. Afisi imeendelea kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo la Afisi pamoja na Ukumbi wa Mikutano wa Sheikh Idriss Abdul Wakil;

v. Imeimarisha mfumo wa mawasiliano wa Afisi kwa kushirikiana na Idara ya Serikali Mtandao ili kuondoa changamoto kwa mifumo ya mawasiliano iliyopo na kurahisisha mawasiliano baina ya Taasisi na wananchi kwa ujumla;

vi. Imeratibu na kuendesha shughuli maalum ya upimaji maradhi mbalimbali ikiwemo UKIMWI, Shindikizo la damu, Sukari na Homa ya Ini kwa wafanyakazi wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

**96. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021Idara ya Uendeshaji na Utumishi kupitia Programu ndogo ya Uongozi na Utawala, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi 1,794,990,000** na kutumia **Shilingi 941,865,813** sawa na **asilimia 52** na **asilimia 69** kwa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa.

***Programu Ndogo – CO10402: Mipango, Sera na Utafiti***

**97. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ambayo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inahusika na uratibu wa masuala ya bajeti, uibuaji na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo pamoja na tafiti zinazohusu masuala yanayosimamiwa na Afisi. Aidha, Programu hii ina jukumu la kuratibu masuala ya sera na miongozo ya sekta iliyomo katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2020/2021 Programu ndogo hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeandaa Mpango kazi wa mwaka 2020/2021, Mpango wa Utekelezaji wa Mpango kazi, Taarifa ya utekelezaji wa Robo ya kwanza, Taarifa ya utekelezaji wa Nusu Mwaka na Taarifa ya Utekelezaji ya Mwaka 2019/2020;

ii. Imeratibu na kufanya tafiti tatu juu ya masuala yanayohusiana na sekta zilizomo Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

iii. Imefuatilia utekelezaji halisi wa miradi ya maendeleo ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa kufanya ziara ya miradi hiyo na kuandaa taarifa na kuziwasilisha sehemu husika;

iv. Imeandaa taarifa ya utekelezaji wa Mpango kazi wa Masuala Mtambuka wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha miezi sita (Julai - Disemba) 2020;

v. Afisi imezipitia Sheria tisa na Kanuni nne zinazohusika na shughuli zinazosimamiwa na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili kubaini changamoto na kutoa mapendekezo ya kuzirekebisha;

vi. Imetoa mafunzo ya uelewa wa Sera na Sheria juu ya masuala ya Watu wenye Ulemavu pamoja na Muongozo wa Kitaifa wa Viwango vya Miundombinu Rafiki, sambamba na kuwaongezea ujuzi wahusika wa utekelezaji wa shughuli za masuala mtambuka katika Idara na Taasisi zilizopo Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

vii. Imetoa mafunzo ya uandishi wa mapendekezo ya awali ya utafiti na maandiko ya taarifa za tafiti kwa Maafisa Mipango wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais;

viii. Aidha, Afisi imeandaa bajeti, mipango ya Afisi pamoja na kuibua miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

ix. Afisi imefanya ufuatiliaji na tathmini za utekelezaji wa programu/ miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Idara/Taasisi zilizomo katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa robo tatu;

x. Afisi imesimamia utekelezaji wa Programu za Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria kupitia chombo cha Uratibu wa Mfuko wa Dunia Zanzibar (ZGFCCM);

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Programu hii Ndogo iliidhinishiwa kutumia Shilingi 473,882,000 kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2021 fedha zilizoingizwa ni Shilingi 242,963,314 ambazo ni sawa na asilimia 51 na asilimia 69 kwa fedha zilizopangwa kutumika miezi tisa.

***Programu Ndogo – CO10403: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi - Pemba***

99. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo inatekelezwa na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Pemba. Kwa vile shughuli zinazofanywa na Idara na Taasisi za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar vilevile hutekelezwa Pemba, Programu hii inahusika zaidi na uratibu wa shughuli hizo kwa Pemba sambamba na shughuli za kiutawala za kila siku. Kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2020/2021. Programu ndogo hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Imeimarisha mazingira ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa upande wa Pemba ikiwemo upatikanaji wa mishahara na stahiki nyengine za wafanyakazi, kuwajengea uwezo wafanyakazi katika masuala ya utunzaji siri na kumbukumbu za Afisi na kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo na kuimarisha miundombinu ndani na nje ya Afisi;

ii. Imeratibu ziara tano (5) na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais;

iii. Imeandaa mipango ya Afisi na bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na taarifa za utekelezaji;

iv. Imeratibu utekelezaji wa mradi wa kijiji cha wananchi walioathirika na mvua za masika ulioko Tumbe ambao umekamilika;

v. Imeratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali Pemba ikiwemo shughuli za TASAF, Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo, na ziara 12 za Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

vi. Imeratibu shughuli za kukabiliana na maafa ikiwemo kutoa elimu kwa jamii juu ya kujiandaa na kukabiliana na maafa na kupokea vifaa vya mradi wa nyumba za maafa, Tumbe ikiwa ni pamoja na vifaa vya hospitali na vifaa vya Skuli ziliopo kwenye mradi huo;

vii. Imeratibu shughuli za maadhimisho ya sherehe za miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar na Maadhimisho ya Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa;

viii. Imeratibu na kusimamia mazishi, usomaji wa hitma na ujenzi wa kaburi la aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Maalimu Seif Sharif Hamad yaliyofanyika kijijini kwao Nyali Mtambwe;

ix. Imeratibu usafirishwaji wa wananchi 14 waliokwenda Dar es Salaam na wananchi 200 waliokwenda Unguja kushiriki katika shughuli ya kuuaga mwili wa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

100. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa **Shilingi 1,027,363,326** kwa matumizi ya kazi za kawaida na hadi kufikia Machi, 2021 Afisi imeingiziwa **Shilingi 711,635,105** sawa na **asilimia 69** na **asilimia 91** kwa fedha zilizopangwa kwa miezi tisa.

## BARAZA LA WAWAKILISHI (C02)

101. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi lina jukumu la kutunga sheria, kufuatilia utendaji wa Serikali na kuidhinisha na kusimamia Mipango ya Maendeleo ya Serikali ili kuhakikisha kuwa mahitaji ya wananchi yanapatikana. Jukumu hili la Baraza linatekelezwa kupitia Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali na Programu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.

**PROGRAMU KUU - (CO201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI NA PROGRAMU KUU – PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

102. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2020/2021 Afisi ya Baraza la Wawakiishi kupitia Programu hizi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Afisi iliratibu mikutano miwili ya Baraza la Wawakilishi, katika mikutano hiyo shughuli mbali mbali zilifanywa ikiwemo chaguzi za viongozi wa Baraza, viapo vya Wajumbe, Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la 10 pamoja na uchaguzi wa viongozi wa Jumuiya mbali mbali zilizoanzishwa ndani ya Baraza. Aidha, Taarifa mbali za Serikali ziliwasilishwa ndani ya Baraza na jumla ya maswali ya msingi 81 na ya nyongeza 201 yaliulizwa. Kwa ufafanuzi wa ziada kuhusu shughuli zilizofanywa ***(Angalia kiambatanisho Namba 4);***

ii. Imeratibu uzinduzi wa Baraza jipya la Wawakilishi la kumi pamoja na kuwaapisha Wajumbe, kufanya uchaguzi wa viongozi wa Baraza (Spika na Naibu Spika). Aidha, baada ya Mkutano huo, Afisi ya Baraza kwa kushirikiana na baadhi ya Taasisi mbali mbali iliwapatia mafunzo Wajumbe wa Baraza kuhusu masuala mbali mbali, yakiwemo masuali yanayohusu shughuli na uendeshaji wa Baraza. Aidha, Afisi imeendelea kuwajengea uwezo wafanyakzi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu ambapo jumla ya wafanyakazi 17 waliendelea na masomo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali;

iii. Imeratibu Shughuli za Kamati ambapo Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi zilifuatilia utendaji wa taasisi za Serikali mwezi wa Januari 2021 kwa Unguja pekee na kwa mwezi wa Machi na Aprili Kamati ziliendelea kufanya kazi Unguja na Pemba;

iv. Afisi iliendelea na kazi ya kuyafanyia matengenezo majengo ya Baraza ya Unguja na Pemba ili kuyaweka katika hali nzuri. Vilevile, Afisi imeanza mchakato wa kuanzisha Baraza Mtandao katika hatua za awali;

103. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Baraza la Wawakilishi kupitia Programu zake mbili kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 21,481,600,000 kwa matumizi ya kawaida ambapo hadi Machi, 2021 jumla ya fedha zilizopatikana ni Shilingi 10,198,524,875 sawa na asilimia 47 au asilimia 72 kwa fedha zilizopangwa kutumika kwa miezi tisa.

## TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR (C03)

104. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina Programu Kuu mbili ambazo ni Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala za Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

### PROGRAMU KUU - (PCO301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI

105. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2020/2021 katika Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi, Tume ya Uchaguzi imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Iliendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kufanya uhamisho wa taarifa, kusahihisha taarifa na kufuta wapiga kura waliokosa sifa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2018.

ii. Iliendesha Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar uliofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kwa uhuru, haki na amani na kwa kutumia fedha kutoka serikalini kwa asilimia 100;

iii. ikiwa ni mwanachama wa Jumuiya mbali mbali za kiuchaguzi za Afrika na Dunia kwa ujumla, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilishiriki uangalizi wa uchaguzi katika nchi ya Uganda na kupata

fursa ya kubadilishana uzoefu wa kufanikisha chaguzi kwa salama na amani, unaozingatia vigezo vya kimataifa.

iv. Kwa Mujibu wa Sheria, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imefanya Uteuzi wa Wajumbe wa Baraza la wawakilishi viti malumu wanawake pamoja na Madiwani wa viti maalumu wanawake katika Manispaa, Mabaraza ya Mji na Halmashauri zote za Unguja na Pemba;

v. Imeendesha chaguzi ndogo kwa ajili ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Pandani na Diwani wa Wadi ya Kinuni. Chaguzi hizo zimetokana na Tume kupokea taarifa ya kuwepo kwa nafasi wazi baada ya wateule wa nafasi hizo kufariki dunia siku chache baada ya kutangazwa kuwa washindi;

vi. Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeendesha mikutano ya Tume ya Uchaguzi na kutekeleza maagizo mbalimbali yanayotolewa na Tume.

vii. Afisi ya Tume ya Uchaguzi imetekeleza kazi mbalimbali za kiutawala ikiwemo kuyafanyia matengenezo majengo yanayotumika na Afisi hiyo katika maeneo mbalimbali.

**PROGRAMU KUU - (CO302): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA ZA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

**106. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha miezi tisa cha mwaka wa fedha 2020/2021, Programu hii ya Usimamizi wa Kazi za Utawala za Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ilitekeleza kazi zifuatazo :-

i. Imekamilisha kuandaa Miundo ya Utumishi na Mishahara kwa wafanyakazi wake na inaendelea na hatua za kuiwasilisha katika mamlaka husika kwa kuidhinishwa;

ii. Imeendesha mikutano ya kawaida ya kila mwezi na ya dharura kila inapotokezea haja ya kufanya hivyo. Vile vile sekretariati

imeendelea kufanya vikao vya kila Jumatatu na Jumatano ya kila wiki sambamba na mikutano maalum ya wafanyakazi wote ili kutathmini utekelezaji wa kazi za Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Mikutano hiyo hufanyika kila baada ya miezi mitatu;

iii. Vilevile, watendaji mbali mbali wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 10 (5 wanaume na 5 wanawake) katika Vyuo Vikuu mbali mbali nchini.

**107.** **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2020/2021, ilipanga kutumia **Shilingi 2,210,700,000** kwa mishahara na kazi za kawaida. Fedha zilizopatikana hadi Machi 2021 ni **Shilingi 1,086,411,315** sawa na **asilimia 49** na **asilimia 63** kwa fedha zilizotengwa kwa miezi tisa.

**UTEKELEZAJI KIFEDHA**

**108.** **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 45,310,282,314** kwa kazi za kawaida na hadi kufikia Machi 2021 imetumia **Shilingi 18,360,134,057** ambazo ni sawa na **asilimia 40** au **asilimia 56** kwa fedha zilizopangwa kutumika kwa miezi tisa. Aidha, Afisi iliidhimishiwa jumla ya **Shilingi 21,783,995,000** kwa kazi za maendeleo na hadi kufika Machi 2021 imepatiwa **Shilingi 1,218,500,000** ambazo ni sawa na asilimia 6 **(Angalia Kiambatanisho Nam. 5 na Nam. 6).**

**109.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi vilevile ilipangiwa kukusanya **Shilingi 125,554,000** na hadi kufika Machi 2021, fedha zilizokusanywa ni **Shilingi 190,986,800** sawa na asilimia 152 **(Angalia Kiambatanisho Namba 7).**

## MAPENDEKEZO YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**110.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi pamoja na taasisi zake kwa mwaka 2021/2022 itatekeleza na kusimamia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14. Kupitia Programu hizo, Afisi imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

### AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS (C01)

**PROGRAMU KUU - (PC0101): URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA PILI WA RAIS**

**111.** **Mheshimiwa Spika,** lengo la Program hii ni kuimarisha utendaji wa kazi kwa Ofisi ya Faragha ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais.

***Programu Ndogo - (C010101): Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais***

**112.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi kupitia Programu hii ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais imepanga kufanya yafuatayo:-

i. Kuratibu ziara 60 za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais za ndani ya nchi na ziara 2 za nje ya nchi;

ii. Kuimarisha ushirikiano na uhusiano mwema wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais kukutana na Mabalozi pamoja na Wageni Mashuhuri;

iii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais anazozitoa kwa wananchi na makundi mbalimbali ya kijamii;

iv. Kuyafanyia kazi malalamiko, migogoro na kero za wananchi kwa kushirikiana na taasisi husika.

v. Kuendelea kufanya matengenezo madogo madogo katika makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais yalioko Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma;

vi. Kuendelea kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4) wa Afisi ya Faragha kwa kiwango cha Stashahada, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Pili pamoja na kuwapatia stahiki nyenginezo wafanyakazi wa Idara.

113. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka 2021/2022 imepanga kutumia jumla ya Shilingi 1,825,256,455 kwa kazi za kawaida ambapo Shilingi 988,302,780 ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na Shilingi 836,953,675 ni kwa matumizi mengineyo.

**PROGRAMU KUU - (C0102): URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI**

114. **Mheshimiwa Spika,** programu hii lengo lake kubwa ni kuweka mfumo imara na endelevu wa uratibu wa shughuli za Serikali, ambapo matarajio ya muda mrefu ni kupatikana kwa huduma bora za Serikali kwa jamii. Programu hii ina programu ndogo nne (4).

***Programu Ndogo – CO10201: Kukabiliana na Maafa***

115. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa ina lengo la kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa kabla, wakati na baada ya kutokea. Kazi za Programu hii zinatekelezwa na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar.

116. **Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamisheni imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu utoaji wa huduma na misaada ya kibinaadamu kwa matukio mbalimbali ya majanga yatakayotokea Unguja na Pemba;

ii. Kutoa elimu ya kukabiliana na maafa kwa makundi mbalimbali ya jamii pamoja na taasisi za Serikali na zisizo za Kiserikali;

iii. Kufanya zoezi la utayari wa kijiandaa na kukabiliana na matukio mbalimbali ya majanga na maafa yanayoweza kutokea;

iv. Kuandaa mikutano na wahusika mbalimbali wa masuala ya kukabiliana na maafa katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Shehia;

v. Kuimarisha Mfumo wa Mawasiliano ya Dharura kwa kufanya matengenezo ya mitambo ya mawasiliano na kuwajengea uwezo watendaji wanaosimamia mfumo;

vi. Kutoa taarifa za tahadhari za mapema kwa jamii juu ya majanga mbalimbali yanayoweza kutokea;

vii. Kufanya ukaguzi katika maeneo 18 yanayotoa huduma kwa jamii kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa mipango na taratibu za kukabiliana na maafa katika maeneo hayo;

viii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli zote zinazotekelezwa na Kamisheni katika ngazi ya Taifa, Wilaya na Shehia;

ix. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4) na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wanne (4) Unguja na Pemba;

**117. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamisheni itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu mbili (2) za maendeleo; (a) Programu ya Kuijengea Uwezo Jamii katika Kujikinga na Kukabiliana na Maafa na (b) Programu ya Kutokomeza Kipindupundu Zanzibar na imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuanzisha mfumo shirikishi wa upokeaji na utunzaji wa taarifa za matukio ya majanga na maafa;

ii. Kuandaa muongozo wa uendeshaji wa Kituo cha Mawasiliano na Operesheni za Dharura; na

iii. Kuchapisha nakala 500 za toleo jipya la Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na Kukabiliana na Maafa wa mwaka 2021.

iv. Kufanya vikao vya kila robo mwaka ya kamati tendaji ya kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kutokomeza Kipindupindu Zanzibar

v. Kufanya vikao viwili vya kamati ya uongozi ya kusimamia Mpango wa Kutokomeza Kipindupindu Zanzibar

vi. Kufanya ziara ya ufuatiliaji wa shughuli zote zinazotekelezwa na taasisi mbalimbali katika kutokomeza kipindupindu Zanzibar.

118. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Kukabiliana na Maafa imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 1,387,000,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 482,000,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 905,000,000** kwa matumizi mengineyo.

***Programu Ndogo – CO10202: Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa***

119. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina jukumu la kuratibu sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na shughuli za kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa. Kazi za Programu hii zinatekelezwa na Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi kupitia Programu ndogo hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha matengenezo ya jengo la Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa lililopo Mwanakwerekwe;

ii. Kuratibu Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964;

iii. Kuratibu ushiriki wa Wananchi na Viongozi katika Maadhimisho ya Sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar pamoja na Sherehe za Uhuru wa Tanzania Bara;

iv. Kuratibu Maadhimisho ya Wiki ya Kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Maadhimisho ya Siku ya Kumbukumbu ya Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume;

v. Kutoa huduma za uuzaji wa Bendera za Zanzibar na za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama yalivyobainishwa kisheria;

vi. Kununua vifaa vya kutolea huduma wakati wa maadhimisho ya sherehe mbalimbali vikiwemo gari ya mizigo, mashamiana, viti, vipoza hewa (AC), magodoro pamoja na mabusati;

vii. Kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu wafanyakazi wanne (4) wa Idara.

120. **Mheshimiwa Spika,** Ili Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa iweze kutekeleza kazi hizo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, tunaomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 1,243,681,493** ambapo **Shilingi 196,992,360** ni malipo ya mishahara ya wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na **Shilingi 1,046,689,133** kwa matumizi mengineyo.

***Programu Ndogo – CO10203: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar***

121. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii ina jukumu la kuratibu shughuli za SMZ, mambo ya muungano, utafiti kitaifa pamoja na kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) hapa Zanzibar. Programu hii ndogo inayotekelezwa na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu na kufuatilia malalamiko ya wananchi yanayowasilishwa katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi na kuratibu ufumbuzi wake katika taasisi husika;

ii. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa ahadi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na kuandaa taarifa ya utekelezaji wake;

iii. Kuratibu na kufuatilia Shughuli za Serikali katika ngazi za Mikoa na Wilaya;

iv. Kuratibu shughuli za utafiti kitaifa;

v. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama Tawala katika Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuandaa taarifa ya utekelezaji wake.

vi. Kuratibu na kufuatilia maelekezo, ushauri, ahadi na m a a g i z o yanayotolewa katika vikao vya Baraza la Wawakilishi;

vii. Kuratibu masuala ya sera kitaifa;

viii. Kuratibu, kuandaa na kushiriki vikao vya masuala ya Muungano;

ix. Kuratibu, kuandaa, kufuatilia na kushiriki vikao vya ushirikiano baina ya Wizara za SMZ na SMT;

x. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo;

**122. Mheshimiwa Spika,** kupitia Progrmu hii ndogo, Afisi itaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu na kusimamia uibuaji wa kaya maskini;

ii. Kuratibu na kusimamia malipo kwa kaya masikini katika shehia za Unguja na Pemba;

iii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kutoa ajira ya muda kwa walengwa wa Mpango;

iv. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya miundombinu; ikiwemo ya afya, maji na elimu;

v. Kuandaa vikao viwili vya Kamati ya Uongozi (Steering Committee) na Kamati Tendaji (Management Committee);

vi. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa TASAF baina ya Zanzibar na TASAF Makao Makuu;

vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa miradi ya TASAF;

viii. Kusimamia uendeshaji wa shughuli za TASAF Unguja na Pemba;

ix. Kuratibu na kusimamia vikundi vya kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya; na

x. Kuratibu na kusimamia mipango ya biashara kwa walengwa wa TASAF.

**123. Mheshimiwa Spika,** Ili Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iweze kutekeleza hayo kwa mwaka 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 694,090,198** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 420,993,660** zitatumika kwa malipo ya mshahara na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na **Shilingi 268,103,121** kwa matumizi mengineyo. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **Shilingi 37,722,600,000** kwa matumizi ya kazi za maendeleo ambapo **Shilingi 100,000,000** ni mchango wa Serikali kwa Mradi/Mpango wa Maendeleo wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF III) na **Shilingi 37,622,600,000** ni mchango wa washirika wa maendeleo.

**124. Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii vilevile naomba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya **Shilingi 16,118,600,000** ikiwa ni ruzuku kwa Idara ya Uhamiaji, Zanzibar.

***Programu Ndogo – CO10204: Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Dodoma***

**125. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dodoma ina lengo la kuimarisha utoaji wa huduma kwa taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya Taasisi/Wizara za SMZ na SMT, Washirika wa Maendeleo, Afisi za Kibalozi na asasi nyengine za kimataifa ikiwemo kuimarisha na kuibua maeneo mapya ya uhusiano na ushirikiano.

126. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu hii ndogo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuratibu na kushiriki vikao 6 vya Afisi za kibalozi;

ii. Kuratibu na kushiriki Vikao vitano (5) vya Taasisi za Jumuiya za Kimataifa;

iii. Kuratibu na kushiriki vikao 80 vya Afisi na Wizara na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iv. Kutoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Watendaji wengine wa SMZ wanapokuwa Tanzania Bara ikiwemo mapokezi, usafiri na urahisishaji wa upatikanaji VISA;

v. Kutoa elimu juu ya uwepo wa Afisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma kwa kufanya warsha moja (1) kwa wadau mbalimbali pamoja na kuandaa Kongomano la Maadhimisho ya Sherehe za Mapinduzi Zanzibar;

vi. Kukamilisha rasimu ya mpango mkakati wa Afisi;

vii. Kuendelea na kufanya utafiti wa tathmini ya utaoji wa huduma za Afisi ya Uratibu Shughuli za SMZ Dodoma;

viii. Kufanya vikao baina ya Maafisa uratibu wa SMZ Dodoma na maafisa viungo wa Wizara na Taasisi mbalimbali za SMZ;

ix. Kuratibu na kurusha vipindi viwili (2) vya ijuwe Afisi ya Uratibu Dodoma kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) na TBC;

x. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi watatu (3) na mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wawili (2);

xi. Kulipia huduma na vifaa vya Afisi.

xii. Kuwapatia wafanyakazi stahiki nyengine.

127. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dodoma itekeleze malengo yake hayo, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 671,107,912** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 410,998,920** kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi na mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na **Shilingi 260,108,992** kwa matumizi mengineyo.

## PROGRAMU KUU - (CO103): UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

128. **Mheshimiwa Spika,** lengo la Programu hii ni kuimarisha mazingira bora ya wafanyakazi, usimamizi wa mipango na shughuli za Afisi ili kutoa huduma bora kwa jamii. Programu hii kuu ina Programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu na Utekelezaji wa Afisi, Pemba.

### *Programu Ndogo – CO10301: Uongozi na Utawala*

129. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina lengo la kuimarisha utendaji kazi wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa kusimamia na kuweka mazingira bora ya kazi na kutoa huduma bora za uendeshaji za kila siku pamoja na kusimamia maslahi na rasilimali za Afisi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 programu ndogo ya Uongozi na Utawala pamoja na mambo mengine, imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea kusimamia maslahi na kuwapatia wafanyakazi stahiki zao zikiwemo mishahara, posho ya likizo, posho la kushika wadhifa, malipo baada ya saa za kazi na stahiki nyinginezo kwa mujibu wa taratibu;

ii. Kuimarisha mazingira bora ya Afisi pamoja na huduma za uendeshaji;

iii. Kuratibu na kusimamia vikao vya uendeshaji vya Afisi vikiwemo vikao vinne (4) vya Kamati ya Uongozi, vikao 12 vya Kamati

Tendaji, vikao vinne (4) vya Kamati ya Ukaguzi na Bodi ya Zabuni;

iv. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kumi (10) wa Idara katika mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 13 mafunzo ya muda mfupi ili kuinua kiwango cha utendaji. Aidha, Programu ndogo hii itaratibu mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 68 na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 196 wa Idara na Taasisi za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

v. Kutoa mafunzo ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, Rushwa na mafunzo juu ya masuala ya uhujumu uchumi na kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI kwa wafanyakazi 300 wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

vi. Kuimarisha kitengo cha ICE kwa kukipatia vitendea kazi vya kisasa;

**130. Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uongozi na Utawala ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2021/2022 inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 1,571,839,909** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 845,543,920** ni kwa malipo ya mishahara na **Shilingi 726,295,989** kwa matumizi mengineyo.

***Programu Ndogo – CO10302: Mipango, Sera na Utafiti***

**131. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti inahusika na kuandaa na kusimamia mipango na bajeti na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ndogo hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti, mipango ya Afisi pamoja na miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

ii. Kuandaa bajeti ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi ya mwaka wa fedha 2022/2023;

iii. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Programu/ miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Idara/Taasisi zilizomo katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

iv. Kuratibu na kusimamia tafiti zinazofanywa na Idara na Taasisi zilizomo katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

v. Kuratibu uandaaji na mapitio sera, sheria na miongozo inayohusu shughuli zinazotekelezwa na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

vi. Kuratibu na kutoa uelewa juu ya masuala mtambuka kwa Idara/ Taasisi zilizopo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

vii. Kuratibu na kuandaa vikao vya mashirikiano baina ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi na Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Makamu wa Rais, SMT;

viii. Kuratibu shughuli za takwimu za Afisi kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Takwimu/Mipango juu ya miongozo ya ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi, uingizaji na uchambuzi wa takwimu kwa kutumia program ya *Statistical Package for Social Science* (SPSS) na matumizi ya taarifa za takwimu;

ix. Kufanya mafunzo juu ya uandaaji wa Bajeti kwa Maafisa Mipango wa Idara/Taasisi zilizopo Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

x. Kufanya tafiti moja (1) juu ya masuala yanayosimamiwa na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi.

132. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 450,331,485** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 180,551,640** ni mishahara na **Shilingi 269,779,845** ni kwa matumizi mengineyo.

***Programu Ndogo – CO10303: Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi Pemba***

133. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Pemba inahusika na kuratibu shughuli za Idara na Taasisi zilizo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi Pemba kwa kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na usimamizi wa shughuli za Afisi. Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Programu hii ndogo imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha mazingira bora ya kufanyia kazi na kusimamia shughuli za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

ii. Kutoa huduma na kuratibu ziara na shughuli za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais anapokuwepo Pemba;

iii. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi sita (6) na muda mfupi wafanyakazi wanne (4) wa Afisi;

iv. Kuandaa mipango na bajeti ya Afisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022;

v. Kuimarisha kazi za usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa program na miradi ya maendeleo iliyo chini ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi;

vi. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali Pemba;

vii. Kuratibu shughuli za kukabiliana na maafa na kutoa elimu kwa jamii juu ya kujiandaa na kukabiliana na maafa;

viii. Kuratibu maadhimisho ya sherehe na maadhimisho ya kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi wakuu wa kitaifa.

134. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu ndogo Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba itekeleze hayo kwa mwaka 2021/2022, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 764,092,544** kwa matumizi ya kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 516,816,720** kwa ajili ya malipo ya mishahara, posho maalum na mchango wa ZSSF na **Shilingi 247,275,824** kwa matumizi mengineyo.

## BARAZA LA WAWAKILISHI (C02)

135. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi linatekeleza Programu kuu mbili ambazo ni Programu Kuu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali na Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi.

**PROGRAMU KUU - (CO201): KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI na PROGRAMU KUU - (CO202): UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

136. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali ina jukumu la kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatelekelezwa Zanzibar, ambapo matarajio yake ya muda mrefu ni kukua kwa demokrasia na uwakilishi wa wananchi. Huduma zinazotolewa ni kujadili, kurekebisha na kupitisha miswada ya Sheria, kusimamia utendaji wa taasisi za Serikali na kujadili na kupitisha bajeti ya Serikali. Aidha, Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kuongezeka kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Baraza na Afisi.

137. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 Baraza la Wawakilishi kupitia Programu hizi limepanga kutekeleza mambo yafuatayo:-

i. Kuratibu mikutano minne (4) ya kila mwaka ya Baraza la Wawakilishi.

ii. Kuratibu shughuli za Kamati za kudumu za Baraza.

iii. Kuendelea kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza ili kukuza ufanisi katika kutekeleza majukumu yao.

iv. Kuendelea kutoa taaluma kwa Umma kuhusu shughuli za Baraza kupitia vipindi vya Redio na T.V .

v. Kuendelea kuimarisha mazingira ya Baraza kwa kufanya matengenezo ya kawaida ya Majengo.

vi. Kuanza matayarisho ya utanuzi wa Jengo la Afisi ya Baraza ili kuondoa changamoto ya uhaba wa nafasi.

138. **Mheshimiwa Spika,** ili Afisi ya Baraza la Wawakilishi iweze kutekeleza malengo yake hayo kwa ufanisi zaidi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 24,337,975,465** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 9,061,432,465** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 15,276,543,000** ni kwa kazi nyenginezo.

## TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR (C03)

139. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inasimamia Programu kuu mbili ambazo ni Programu ya Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi na Programu ya Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**PROGRAMU KUU - (CO301): UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI**

140. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu ina jukumu la kukuza demokrasia na umoja wa kitaifa kwa kuwa na uchaguzi huru na wa haki na wenye kufuata misingi ya kisheria. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendeleza Daftari la Kudumu la Wapiga Kura;

ii. Kuendelea kutoa elimu ya wapiga kura kwa makundi mbali mbali.

iii. Kuendesha chaguzi ndogo zitakapotokezea;

iv. Kutoa elimu ya Uchaguzi kwa Wajumbe na Watendaji wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

141. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi fedha zake zinatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**PROGRAMU KUU - (CO301): USIMAMIZI WA KAZI ZA UTAWALA NA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA TUME YA UCHAGUZI YA ZANZIBAR**

142. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuimarisha usimamizi wa mwenendo wa shughuli za uchaguzi, ambayo matarajio yake ya muda mrefu ni uendeshaji bora wa kazi za Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Programu hii inasimamia program mbili ambazo ni :-

i. Usimamizi wa kazi za utawala na uendeshaji wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

ii. Usimamizi wa kazi za Utawala na Uendeshaji wa Afisi Ndogo ya Tume ya Uchaguzi Pemba.

143. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii imepenga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuimarisha majengo ya Afisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa Wilaya ya Kaskazini 'B' na Kusini.

ii. Kuendelea kutoa fursa za kujiendeleza kitaaluma kwa wafanyakazi katika ngazi mbali mbali za elimu.

iii. Kujaza nafasi mbali mbali za watendaji zilizowazi kutokana na kustaafu na uhamisho wa watumishi.

iv. Kununua vifaa pamoja na huduma mbali mbali kwa ajili ya kuleta ufanisi katika Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

v. Kutoa elimu ya Uchaguzi kwa Wajumbe na Watendaji wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

144. **Mheshimiwa Spika,** ili Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iweze kutekeleza malengo yake hayo kwa ufanisi zaidi, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe **Shilingi 2,248,900,000** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 1,518,100,000** ni kwa ajili ya malipo ya mishahara na **Shilingi 730,800,000** ni kwa matumizi mengineyo.

145. **Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, makisio kwa Programu zote 7 za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni **Shilingi 89,030,482,044** kwa kazi za kawaida ambapo **Shilingi 14,621,732,465** ni za mshahara, **Shilingi 36,686,149,579** ni kwa matumizi mengineyo na **Shilingi 37,622,600,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo **(Angalia Kiambatanisho Nam. 8).**

## UKUSANYAJI MAPATO

146. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Taasisi zake imepangiwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 171,315,000** kwa mchanganuo ufuatao:-

| | |
|---|---|
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 49,422,100 |
| Afisi Kuu Pemba | 21,180,900 |
| Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | 100,712,000 |
| **Jumla** | **171,315,000** |

**HITIMISHO**

**147. Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, natumia fursa hii ya pekee kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambayo katika kipindi hiki kifupi imefanya kazi zake kwa ukaribu sana na Afisi yetu. Naishukuru pia kwa kuipitia hotuba yetu hii na kutushauri ipasavyo na hatimae kuridhia kuwasilishwa katika Baraza hili. Kwa upande wetu tunaahidi kuendelea kushirikiana nayo na kufanya kazi zetu kwa pamoja ili kufikia lengo la kuwahudumia wananchi wetu.

**148. Mheshimiwa Spika,** vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wadau mbalimbali wa ndani na nje walioshirikiana na Serikali katika kutoa huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tumeshuhudia miradi na shughuli nyingi zikitekelezwa katika Wizara na taasisi zetu kwa mashirikiano makubwa na Washirika wa Maendeleo. Miongoni mwa washirika hao ni:- Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mashirika ya Umoja wa Mataifa ikiwemo UNDP, UNICEF, UNFPA, WHO, WFP, UNAIDS, USAID, FAO, Mfuko wa Dunia wa Kupambana na Kifua Kikuu Malaria na UKIMWI, Nchi za China, India, Japan, Marekani, Oman, Umoja wa Falme za Nchi za Kiarabu (UAE), Cuba na nyenginezo. Tunawaomba Washirika wetu hao kuendelea kushirikiana na Serikali katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

**149. Mheshimiwa Spika,** Pia nazishukuru sana Afisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Afisi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo tunafanya kazi kwa pamoja katika masuala mbalimbali ya kitaifa.

150. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunazishukuru sana Taasisi, Mashirika ya kitaifa pamoja na wafanyabiashara ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi katika shughuli za kijamii. Nawaomba waendelee kuchangia kadri hali inavyoruhusu ili kwa pamoja kuweza kufikia lengo letu la kuwahudumia wananchi kwa ubora wa hali ya juu.

151. **Mheshimiwa Spika,** pia, tunawashukuru waandishi wa habari wa vyombo vyote nchini kwa kusaidia kutoa taarifa mbalimbali za kimatukio na za kuelimisha kwa jamii yetu. Nawaomba waendelee kutoa taarifa kwa umakini zaidi kutoka kwenye vyanzo husika bila ya kufuata utashi wa mtu au taasisi.

152. **Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu naomba sana nichukue fursa hii kumshukuru kwa dhati msaidizi wangu wa shughuli za kiofisi Mheshimiwa Dkt. Khalid Salum Mohamed, Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano makubwa anayonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kuisimamia Afisi hii na katika utoaji wa huduma kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, naishukuru sana timu ya watendaji wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Thabit Idarous Faina, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizomo katika Afisi hii pamoja na watendaji wote. Hakika ninafarijika sana na uwezo na jitihada zao wote katika kuifanya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awajaalie maarifa, nguvu na uwezo zaidi wa kutekeleza majukumu yao kwa manufaa ya nchi yetu.

153. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine tena napenda kuwakumbusha wananchi wote kuendelea na kujitahidi kufuata maelekezo yanayotolewa na Serikali pamoja na wataalamu wa afya katika kujikinga na maambukizo ya maradhi mbalimbali vikiwemo virusi vya COVID – 19, matumbo ya kuharisha na kipindupindu hasa katika kipindi hiki cha

mvua. Tuendelee kuchukua jitihada za kuyaweka maeneo yetu safi na kufuata maelekezo ya wataalam wa afya.

154. **Mheshimiwa Spika,** kwa vile tumo katika mfungo wa mwezi wa Ramadhan napenda kuwatakia waislamu wenzangu wote Mfungo Mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Niwakumbushe ndugu wananchi kuendelea kufanya ibada na kuliombea Taifa letu lizidi kuwa na amani na utulivu.

155. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 89,030,482,044** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi na Taasisi zake kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 nilizozielezea hapo awali. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| C01 - Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais | Shilingi | 62,443,606,579 |
| C02 - Afisi ya Baraza la Wawakilishi | Shilingi | 24,337,975,465 |
| C03 - Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | Shilingi | 2,248,900,000 |
| **JUMLA KUU** | **Shilingi** | **89,030,482,044** |

156. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

MHE. HEMED SULEIMAN ABDULLA
**MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR**

# VIAMBATANISHO

**KIAMBATISHO NAM. 1**

## WAFANYAKAZI WALIOPATIWA STAHIKI NYENGINEZO KWA MWAKA 2020/2021

| JINA LA IDARA/TAASISI | MALIPO YA POSHO LA LIKIZO | | MAREKEBISHO YA MSHAHARA | | KUTHIBITISHWA KAZINI | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | F | M | F | M | F |
| Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais | - | 2 | 7 | 7 | 1 | 4 |
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 3 | 3 | 1 | 1 | 3 | 1 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 |
| Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali | 2 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 |
| Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 0 |
| Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 3 | 0 | 2 | 3 | 0 | 0 |
| Ofisi Kuu – Pemba | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 | 3 |
| **JUMLA KUU** | **8** | **7** | **11** | **14** | **13** | **9** |

**KIAMBATISHO NAM. 2. IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MUDA MREFU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

| JINALA IDARA/TAASISI | CHETI (CERTIFICATE) | | STASHAHADA (DIPLOMA) | | SHAHADA YA KWANZA (DEGREE) | | STASHAHADA YA UZAMILI (PGD) | | SHAHADA YA PILI (MASTERS) | | SHAHADA YA UZAMIVU (PhD) | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **M** | **F** | **M** | **F** | **M** | **F** | **M** | **F** | **M** | **F** | **M** | **F** | |
| Ofisi ya Faragha ya Makamu wa Pili wa Rais | - | 2 | - | 1 | | 3 | - | - | 2 | 1 | - | - | 9 |
| Idaraya Uendeshaji na Utumishi | 1 | 2 | - | 2 | 1 | 3 | - | - | 3 | - | - | - | 12 |
| Idaraya Mipango, Sera na Utafiti | - | 1 | - | - | - | - | - | - | 1 | 3 | 1 | - | 6 |
| Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali | - | 1 | - | 1 | - | - | - | - | 3 | 6 | - | - | 11 |
| Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dodoma | - | - | - | - | - | 1 | - | - | - | 3 | - | - | 4 |
| Idaraya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | - | - | - | - | - | 2 | - | - | - | 1 | - | - | 3 |
| Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | - | - | 1 | - | 2 | 3 | - | - | 1 | - | - | - | 7 |
| Ofisi Kuu – Pemba | - | - | 1 | 6 | - | - | - | - | 3 | - | - | - | 10 |
| **JUMLA KUU** | | **6** | **2** | **11** | **3** | **12** | **-** | **-** | **13** | **14** | **1** | **-** | **62** |

**KIAMBATISHO NAM. 3**

**IDADI YA WAFANYAKAZI WALIOPATIWA MAFUNZO YA MAALUM KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

| NAM. | AINA YA MAFUNZO | IDADI YA WAFANYAKAZI | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| | | WANAWAKE | WANAUME | |
| 1 | Mafunzo ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | 135 | 137 | 272 |
| 2 | Mafunzo elekezi kwa Watumishi Wapya | 13 | 13 | 26 |
| 3 | Mafunzo ya Sheria ya utumishi wa umma ya mwaka 2014 | 93 | 94 | 187 |
| | **JUMLA KUU** | **241** | **244** | **485** |

**KIAMBATANISHO NAM. 4**

## UTEKELEZAJI WA SHUGULI ZA BARAZA

| SHUGHULI | UTEKELEZAJI | |
|---|---|---|
| Shughuli wa Kwanza wa Baraza la Wawakilishi wa tarehe 8/11/2020 – 11/11/2020 | i. | Uchaguzi wa Spika na Naibu Spika |
| | ii. | Viapo vya Wajumbe |
| | iii. | Hutuba ya Uzinduzi wa Baraza la 10 iliyotolewa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk Hussein Ali Mwinyi. |
| Shughuli zilizotekelezwa katika Mkutano wa Pili wa Baraza tarehe 10/2/2021-25/2/2021 | i. | Kuwasilishwa Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka 2019/2020. |
| | ii. | Kuwasilishwa Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mawizara na Mashirika kwa mwaka 2018/2019. |
| | iii. | Kuwasilishwa Ripoti ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar mwaka 2020. |
| | iv. | Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza la Kumi la Wawakilishi aliyoitoa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 11/11/2020. |

| SHUGHULI | UTEKELEZAJI |
| --- | --- |
| | *v.* Mjadala wa Mwelekeo wa Mpango wa Taifa kwa mwaka 2021/2022 na Waraka wa Mpango wa Bajeti *(Budget Framework Paper).* |
| | vi. Marekebisho ya Jadweli ya Pili ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, Sheria Nam. 4 ya 2015. |
| | vii. Kuwasilisha Barazani Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388, *"Revised Edition" (RE)* 2020 kwa mujibu wa Kifungu cha 132 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984. |
| | viii. Mswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria Mbali Mbali. |
| | ix. Uchaguzi wa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. |
| | x. Uchaguzi wa Wabunge watano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar. |
| | xi. Uchaguzi wa Umoja wa Wanawake wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. |
| | xii. Uchaguzi wa Viongozi wa Chama cha Wabunge wa Nchi za Jumuiya ya Madola Kanda ya Zanzibar *(CPA).* |

| SHUGHULI | UTEKELEZAJI |
|---|---|
| | *xiii.* Uchaguzi wa Chama cha Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola, Kanda ya Zanzibar *(CWP).* |
| | xiv. Uchaguzi wa Viongozi wa Umoja wa Wawakilishi wa Kupambana na Ukimwi Zanzibar (UWAKUZA). |
| Mafunzo mbali mbali Yaliyotolewa kwa njia ya Warsha | i. Semina kuhusu masuala ya Kupambana na Rushwa na Mtandao wa Wabunge wa Kupambana na Rushwa Afrika *(APNAC).* |
| | ii. Semina kuhusu Mabadiliko ya Tabia Nchi. |
| | iii. Semina kuhusu Protokali za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. |
| | iv. Semina kuhusu Chama cha Mabunge ya Nchi za Jumuiya ya Madola, Kanda ya Zanzibar *(CPA).* |
| | v. Semina kuhusu Chama cha Wabunge Wanawake wa Nchi za Jumuiya ya Madola, Kanda ya Zanzibar *(CWP).* |
| | vi. Semina kuhusu Umoja wa Wawakilishi wa Kupambana na Ukimwi Zanzibar (UWAKUZA). |

**KIAMBATANISHO NAM. 5**

**TAARIFA YA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 HADI MACHI, 2021**

| Na. | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA ( %) KWA MIEZI TISA | ASILIMIA (%) KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1.Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | 1.Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais | Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais | 1,443,495,314 | 752,487,324 | 900,844,423 | **120** | **62** |
| 2 | Uratibu wa Shughuli za Serikali | 2. Kukabiliana na Maafa | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 1,086,826,000 | 822,601,000 | 537,633,405 | **65** | **49** |
| | | 3. Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa | Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 1,270,817,000 | 1,203,546,116 | 498,304,293 | **41** | **39** |
| | | 4. Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ | 750,757,000 | 534,272,203 | 443,814,163 | **83** | **59** |
| | | | Ruzuku kwa ajili ya Shughuli za Idara ya Uhamiaji | 14,100,000,000 | 10,575,000,000 | 2,395,000,000 | **23** | **17** |

| Na. | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA ( %) KWA MIEZI TISA | ASILIMIA (%) KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 5. Shughuli za SMZ Dar es Salaam | Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, Dar es Salaam | 669,852,000 | 520,994,962 | 403,137,351 | **77** | **60** |
| 3 | Uendeshaji na Uratibu | 6. Uongozi na Utawala | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 1,794,990,000 | 1,363,126,405 | 941,865,813 | **69** | **52** |
| | | 7. Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 473,882,000 | 354,608,214 | 242,963,314 | **69** | **51** |
| | | 8. Ofisi Kuu Pemba | Ofisi Kuu Pemba | 1,027,363,000 | 786,010,110 | 711,635,105 | **91** | **69** |
| 4 | Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | 9. Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali | Baraza la Wawakilishi | 8,428,646,000 | 14,110,883,900 | 10,198,524,875 | **72** | **47** |
| 5 | Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | 10.Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi | | 9,860,741,000 | | | | |
| | | 11. Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba | | 3,192,213,000 | | | | |

| Na. | JINA LA PROGRAMU | JINA LA PROGRAMU NDOGO | IDARA/TAASISI HUSIKA | MAKISO KWA MWAKA | MAKISIO KWA MIEZI TISA | FEDHA ILIYOPATIKANA KWA MIEZI TISA | ASILIMIA ( %) KWA MIEZI TISA | ASILIMIA (%) KWA MWAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Uendeshaji wa Shughuli za Uchaguzi | 12.Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Uchaguzi | Tume ya Uchaguzi | - | | - | - | |
| 7 | Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar | 13. Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Unguja | | 2,210,700,000 | 1,736,709,750 | 1,086,411,315 | **63** | **49** |
| | | 14. Uendeshaji wa shughuli za kiutawala wa Tume ya Uchaguzi Pemba | | | | | | |
| | | | | **46,310,282,314** | **32,760,239,984** | **18,360,134,057** | **56** | **40** |

**KIAMBATANISHO NAM 6**

**UPATIKANAJI WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI, 2020 HADI MACHI, 2021**

| S/N | JINA LA PROGRAMU NDOGO | JINA LA MRADI | FEDHA ILIYOTENGWA KWA MWAKA | | FEDHA ILIYOPATIKANA | ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kukabiliana na Maafa | Mradi wa kujenga uwezo wa Kukabiliana na Maafa | Wahisani | 186,000,000 | 186,000,000 | 100 |
| | | | SMZ | - | - | |
| 2 | Shughuli za SMZ | Programu ya TASAF III | Wahisani | 21,547,995,000 | 982,500,000 | 5 |
| | | | SMZ | 50,000,000 | 50,000,000 | 100 |
| | | | | **21,783,995,000** | **1,218,500,000** | **6** |

KIAMABATANISHO NAM. 7

## UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 - MACHI, 2021

| IDARA/TAASISI | FEDHA ILIYOTENGWA | FEDHA ILIYOKUSANYWA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa | 62,800,000 | 24,297,800 | 39 |
| Ofisi Kuu Pemba | 5,254,000 | 2,880,000 | 55 |
| Tume ya Uchaguzi | 57,500,000 | 163,809,000 | 285 |
| | **125,554,000** | **190,986,800** | **152** |

**KIAMBATANISHO NAM. 8**

## MAKADIRIO YA FEDHA KWA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA NA MAENDELEO

## KWA MWAKA 2021/2022

| IDARA/TAASISI | MSHAHARA | OC | MAENDELEO SMZ | MAENDELEO WAHISANI | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| FARAGHA | 988,302,780 | 836,953,675 | - | - | **1,825,256,455** |
| SHEREHE | 196,992,360 | 1,046,689,133 | - | - | **1,243,681,493** |
| URATIBU SMZ | 420,993,660 | 268,103,121 | 100,000,000 | 37,622,600,000 | **38,411,696,761** |
| URATIBU DOM | 410,998,920 | 260,108,992 | - | - | **671,107,912** |
| U/ UTUMISHI | 845,543,920 | 726,295,989 | - | - | **1,571,839,909** |
| MIPANGO | 180,551,640 | 269,779,845 | - | - | **450,331,485** |
| PEMBA | 516,816,720 | 247,275,824 | - | - | **764,092,544** |
| **Jumla ndogo** | **3,560,200,000** | **3,655,206,579** | **100,000,000** | **37,622,600,000** | **44,938,006,579** |
| Ruzuku | | | | | |
| MAAFA | 482,000,000 | 905,000,000 | - | 0 | 1,387,000,000 |
| UHAMIAJI | - | 16,118,600,000 | - | - | 16,118,600,000 |
| **Jumla ndogo** | **482,000,000** | **17,023,600,000** | **-** | **0** | **17,505,600,000** |
| **JUMLA KUU (C01)** | **4,042,200,000** | **20,678,806,579** | **100,000,000** | **37,622,600,000** | **62,443,606,579** |
| BARAZA LA WAWAKILISHI | 9,061,432,465 | 15,276,543,000 | - | - | **24,337,975,465** |
| TUME YA UCHAGUZI | 1,518,100,000 | 730,800,000 | - | - | **2,248,900,000** |
| **JUMLA KUU - AMPR** | **14,621,732,465** | **36,686,149,579** | **100,000,000** | **37,622,600,000** | **89,030,482,044** |